

KIMULIMULI CHEKUNDU CHA

DALILI YA KUJA KWAKE



Asante Ndugu Neville. Hebu na tuendeleo kusimama kidogo kwa maombi, na tuinamishe vichwa vyetu. Baba yetu wa Mbinguni, Kwako twatoa sifa kwa mambo yote ambayo macho yetu yameona na masikio yetu yamesikia. Na twakushukuru Wewe, Bwana, kwa sababu leo tunajua kwamba Wewe ni Yehova Mungu yeye yule aliye mkuu na atakayekuwa daima.

² Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya Yesu Kristo Ambaye amewezesha tupate kurudi kwenye ushirika wa Kiungu pamoja Nawe tena, kwa njia ya kumwagika kwa Damu Yake isiyo na hatia, kwamba kupitia u—upatanisho wa Damu hiyo sisi sasa ni wana na binti za Mungu. Haijadhihirika bado tutakavyokuwa mwishoni, lakini twajua tutafanana Naye, kwa maana tutamwona Yeye kama alivyo. Basi, Baba, hilo latutosha kabisa, maadamu tunafanana na Yeye, tukisimama katika umbo la mfano Wake.

³ Na sasa, Baba, hatutaki wakati huu kuyafuatisha mambo ya ulimwengu, bali tugeuzwe kwa kufanywa upya roho zetu, kwa Roho Mtakatifu, Yeye apate kuja akachukue maisha yetu katika ulinzi Wake Mwenyewe, na a—apate kutuongoza na kutuelekeza katika siku tulizobakiza duniani, nasi tukalitukuze Jina Lake kuu.

⁴ Tunakushukuru Wewe kwa mambo haya yote. Na kwa matazamio tunakutazamia kuzuru Kwako pamoja nasi usiku wa leo tukiwa tumekusanyika humu ndani sasa, na tukiamini kwamba Wewe utakutana nasi kama ulivyoahidi. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ketini.

⁵ Naamini ni Daudi aliyesema, “Nilifurahi walipotuambia, waliponiambia, ‘Na twende katika nyumba ya Bwana.’” Basi tunakushukuru sana kuwapo hapa usiku wa leo, na ni majaliwa kuwa na nafasi hii nzuri sana ku—kuwepo hapa, kuzungumza nanyi watu.

⁶ Ninarekodi kanda chache. Kwa hiyo nimeangalia kule nyuma chumbani kuona iwapo ndugu wanachukua kanda. Ina—inaendelea sasa, kanda zinaendelea. Sawa. Kusudi la jambo hili, ni kwamba, niliahidi kupeleka Jumbe, ningekuja, nirekodiwe hapa Maskanini. Sasa tuna . . .

⁷ Ningetaka kusema jambo fulani kuhusu asubuhi hii. Leo, mara tu baada ya adhuhuri, hasa, tulipokuwa tunamaliza

mkutano wa asubuhi, jambo fulani lilitukia ambalo labda baadhi yenu hamkuwepo na hamkusikia habari zake. Nilikuwa ninafunga ibada, nami nilikuwa nikizungumza toka hapa jukwaani, nikimwalia ndugu akisimama hapa akipeana mikono na watu, jina lake Ndugu Way, tunavyomwita yeye hapa. Mkewe ni nesi aliyehitimu.

⁸ Na Ndugu Way ni mmoja wa watumishi wa Mungu, naye pia hufanya kazi ya serikali, lakini ana wito moyoni mwake, kwa miaka mingi, wa kazi ya umishenari. Alijisikia ameongozwa kwamba Mungu angemleta hapa apate kungoja penye kituo hiki hapa hata atakapopokea maagizo zaidi kuingia katika huduma. Siku chache zilizopita, nikizunguma naye, nilipokuwa na mahojiano madogo naye pamoja na mkewe.

⁹ Na asubuhi hii, nilipokuwa ninakiri kwamba nina kinyongo, nilimtaja Ndugu Way pia kwamba ana kinyongo, jambo ambalo bila shaka ni la kawaida miongoni mwa watu wote, na mu—muda mfupi baadaye, Ndugu Way alishikwa na ugonjwa mbaya wa moyo akaanguka sakafuni akafa. Nami nilimwona mkewe, na nikaona... Nimeshuhudia watu wengi wakifa, na ha—hainibidi ku—kusema jambo hili.

¹⁰ Napenda kujivunia Yesu Kristo, na nguvu Zake. Bali wakati huu nafikiri haitupasi kujaribu kamwe kujivunia Yeye kwa njia yo yote kwa jambo ambalo Yeye—Yeye hakutenda. Bali nimemwona Yesu Kristo akifufua wafu, mara nyingi, thabiti kabisa, madaktari wakifanya majaribio kuhakikisha.

Kwa mfano, huko Connecticut hivi majuzi, katika mkutano mmoja, tukiketi katika namna fulani ya ukumbi, mkubwa... maarufu wa mkutano, alikuweco Daktari Barton, daktari Mkristo jukwaani pamoja nami, daktari wa madawa. Na palikuwa na mwanamke mzuri maarufu Mkristo, mwanamke mzuri, alikuwa tajiri sana. Alikuwa ameketi kuelekea mkono wangu wa kushoto. Nami nilikuwa nimefanyiza mstari wa maombi, ndipo nikamwona yule mwanamke mara moja...

¹¹ Wakati mtu ye yote, moyo wake unaposimama... Unaweza ufumbe macho yako, bali wakati unaposhtuliwa nusura kufa, wakati moyo wako unaposimama, kwa kweli mboni zako za macho hupinduka nyuma, na ile sehemu nyeupe ya jicho lako hutokeza nje. Nami nililishuhudia jambo hilo wakati alipokuwa anaanguka chini. Na haraka sana walimwita yule daktari wa madawa, naye akamwendea haraka kupima mapigo yake, ndipo akatikisa kichwa chake, akaweka mikono yake juu yake, sikio lake kwenye moyo wake. Naye alikuwa ameshaaga dunia. Alianguka sakafuni, huku binti yake akipiga makelele, jambo ambalo liliukatiza mkutano. Niliendelea, sababu sikuwa na Neno lo lote la Bwana kwa yule mwanamke. Basi nikaendelea.

¹² Walisema kitu kama kumwita Ndugu Branham. Nao wakasema, “Hatutaki kumwita akiwa kwenye mstari wa

maombi, sababu yuko chini ya utambuzi.” Kisha wakasema, “Mwite Branham mdogo,” huyo alikuwa Billy. Naye Billy, kwa vile ilikuwa ni mwanamke aliyekufa, hakutaka kwenda.

¹³ Unajua, watu huona shaka juu ya mtu aliyekufa. Hilo, hilo ni—hilo ni ganda tu. Hakuna kitu hapo. Hapo, watu huwazia vya ajabu. Huyo, mtu huyo hayupo hapo, mwenyewe, wameenda zao. Na kwa hiyo aliogopa ku—kumkaribia yule mwanamke, kwa sababu amekufa.

¹⁴ Ndipo mara Roho Mtakatifu akanena nami. Nikaondoka mahali pale, nikashuka chini kwa vipandio, nikaja alipokuwa. Na nilipoanza kwenda tu alipokuwa, Roho Mtakatifu akanena nami. Ndipo nikasema, “Mary!”

¹⁵ Akasema, “Naam, Ndugu Branham.” Alikuwa mzima. Na—na hajawahi kutuona sisi hapo kabla. Na ilikuwa mara ya kwanza mkutanoni.

¹⁶ Halafu huko Shawano hivi majuzi yapata, loo, ningesema, isiyopungua, kama, miaka minne iliyopita, au mitano. Nilikuwa nikizungumza usiku mmoja kwenye ghala ya silaha. Na palikuwa na kundi kubwa la watu. Na mzee mmoja wa yapata miaka themanini, nadhani, na mke wake wa kupendeza, walikuwa wa dini ya Kiluteri, wanahudhuria lile kanisa maarufu la Kiluteri pale. Ninalisahau jina lake sasa. Ndilo kusanyiko kubwa sana la Kiluteri Amerika, kwenye kusanyiko moja, kwa washiriki wa kanisa. Na ni nchi maarufu kwa Mluteri. Na nilipokuwa nikizungumza, nilimwona mtu yule, kichwa kikirudi nyuma namna hiyo; na mikono yake ikainama, naye akaanguka kifudufudi, akafa kitini. Ndipo mkewe akaanza kupiga kelele, akapaza sauti, “Jamani nisaidieni! Jamani nisaidieni!”

¹⁷ Na nikaangalia. Nikasema, “Hebu kila mtu aketi, nyamazeni.” Unaona? Nilimngoja Bwana anipe neno. Na—nami. . . Shetani. . . Nilikuwa tu ninajitayarisha kutoa mwito wa madhabahuni, na hapo ndipo tu anapotaka kujionyesha.

¹⁸ Kwa hivyo uliwahi kuchunguza wakati unapoanza kutoa mwito wa madhabahuni, hata vitoto vichanga vitaanza kupiga makelele, na mambo kama hayo? Huyo ni Shetani. Ninyi ambao ni wa rohani mnaelewa.

¹⁹ Kwa hiyo Bwana alinipa jina lake, nami nikamwita, naye akafufuka *hivyo*.

²⁰ Na asubuhi hii nilipokuwa ninageuka, unaona, na nimeona, mara nyingi, Bwana Yesu akiwafufua wafu. Yule mtoto mchanga kule Mexico alikufa kwenye saa tatu asubuhi ile, na hii ilikuwa kati ya saa nne na saa tano usiku ule huyo alipofufuka. Na—na huo ni ushuhuda uliothibitishwa pamoja na ushuhuda wa daktari wa jambo hilo, unaona, kwamba huyo mtoto alikufa katika ofisi yake kwenye saa tatu asubuhi ile. Nafikiri ilikuwa niumonia. Na mtoto huyo anaishi leo, kadiri nijuavyo

mimi. Na hilo lilikuwa mbele, loo, jamani, ya watu thelathini, arobaini elfu.

²¹ Ndipo asubuhi hii nilimwona Ndugu yetu Way, kama anavyoketi, alikuwa ameketi papa hapa sasa. Lakini alivyokuwa anaketi papa hapa mahali fulani ndani *humu*, alikuwa amesimama. Nasi tulikuwa tunaimba, na, “Utukufu, utukufu, haleluya,” na kupeana mikono. Nilimwona wakati ulipokuwa unamshika, na kichwa kikarudi nyuma. Yeye, Ndugu Way, hana ugonjwa wa vitu kama kuzimia au kufanya hivyo. Basi, yeye, nilimwona akianguka kichalichali. Kisha nikamuona mkewe, ambaye ni nesi aliyehitimu, akichunguza mapigo yake ya moyo. Ndipo akapiga makelele; yalikuwa yamekoma.

²² Ndipo—ndipo naamini ilikuwa Dada Nash, bibi hapa, dada mweusi anayekuja kanisani, baadhi yao walianza kukimbia mbele. Na sasa yeye, Bibi Way, aliendelea kunipungia mkono nitoke pale jukwaani nje. Nami nikasema, “Kila mtu anyamaze kimya, msiondoke vitini mwenu.” Msihangaike kamwe katika nyakati kama hizo. Unaona? Hilo ndilo Shetani anataka mfanye. Subiri tu uone ambalo Yeye atasema. Kama ni mtu fulani anaenda Utukufuni, vema, hatuna budi kwenda siku moja, hapana mahali pazuri kuliko kanisani, kwa hiyo—kwa hiyo basi mumo humo katika nyumba ya Bwana. Kwa hiyo basi . . .

Lakini huyo mtu alikuwa anageuka nyuma. Nikafikiri pengine jambo fulani basi, amezimia au jambo fulani limempata, la namna hiyo. Bali nilipotazama, na kichwa chake kimegeuzwa namna *hii*, pia nilipoona mle ndani, sehemu ya chini ya macho yake, imetokeza nje. Huwezi kufumba, huwezi kuweka macho yako katika hali ile, kusimama kwa moyo ndiko kunafanya hivyo. Nami nikapita *hii*, naye . . . Kulikuwa na mtu fulani, mtu mkarimu, alitandika . . . kitu fulani cha kulazia kichwa chake. Hiyo hapo miguu yake, mikono, na kila kitu, vimekakamaa. Ulisimama. Uso wake ulikuwa mweusi kama koti langu, wekundu mweusi, na macho yake yamepinduka nyuma. Nami najua ugonjwa mbaya wa moyo. Najua wanavyofanya na jinsi wanavyogeuka; mtu mwingine ye yote aliyewahi kuuona. Kwa hiyo niliweka mkono wangu kwenye mapigo ya moyo wake, na hakuna mapigo tena zaidi ya yalivyo katika dawati hili. [Ndugu Branham anagonga mimbara ya mbao—Mh.] Hamna kitu. Mkewe yupo hapa, nesi aliyehitimu, aliyechunguza mapigo yake ya moyo. Hapakuwepo na mapigo ya moyo mle.

²³ Basi, juzijuzi nilipokuwa na Ndugu Way kwenye utambuzi humu ndani, niliona kwamba alikuwa na moyo unaonong’ona, hata hivyo. Kwa hiyo basi nikawaza, “Haya basi.” Kwa hiyo niliweka mikono yangu juu yake. Nikasema, “Mungu mpenzi, ninaita, katika Jina Lake Yesu Kristo, nafsi ya ndugu yangu, uhai wake urudi tena.” Na Bwana Yehova anajua, na Biblia Yake ikiwa mbele yangu, ilisikika kama, nilipouweka mkono wangu kwenye mapigo yake ya moyo . . . Na kama nijuavyo nitawajibika

katika jambo hili Siku ya Hukumu kama ni makosa. Basi ilisikika kama mapigo ya moyo wake yalipiga mara nne au mara tano, haraka, yakafanya, tutu, tutu, tutu, tutu, tutu; na kisha ukaanza, ukienda, *tutu, tutu, tutu, tutu*.

²⁴ Naye alikuwa anataka kufungua mdomo wake kuniambia jambo fulani. Na kujaribu kufanya mdomo wake, na kugugumiza, kwa namna fulani, akijaribu kutamka hilo. Ndipo akatamka maneno, “Ndugu Branham.” Kisha ikaonekana kama kwamba angerudi usingizini au jambo fulani, basi nikangojea kidogo tena, nikayachunguza mapigo yake tena; yalikuwa yanapiga kawaida. Na halafu tena nikaangalia, naye akanitazama. Naye alikuwa kwa namna fulani, niliona, hajifahamu; hakujuu alipokuwa, ila moyo wake ulipiga kawaida. Naye Mungu alikuwa amemrudishia uhai wake tena.

²⁵ Kwa hiyo na—nasema hilo kwa heshima ya Yesu Kristo, ambaye ni Mungu yeye yule, kwamba wakati... Asubuhi hii nilihubiri kwa kirefu, nikapita wakati wangu kabisa, nimechoka na kudhoofika. Na kungewezekana kuwe na mambo mawili. Au alichoka, au nilipozungumzia juu ya kuwa na kinyongo, siyo tu kumuumbua ndugu yangu, kama vile tungenema, kwa sababu nilikuwa... ninakiri kwamba nina kinyongo. Na nadhani kama ningaliuliza usiku wa leo, katika kundi hili la watu wanaosikiliza, “Ni wangapi ndani humu mnajua mna kinyongo?” karibu kila mkono ungeinuliwa juu. Ili ujue, Ndugu Way, hebu nikuonyeshe kama ni utambuzi au la. Wangapi mnajua kama mna kinyongo, inueni mikono yenu. Angalia hapo! Unaona? Lakini si—sijui kama mshtuko huo wa kumwambia Ndugu Way jambo hilo, akalichukua kama kwamba ninamkemea au jambo fulani, basi, ndiyo sababu aliingia katika hali hii, kisha Bwana Yesu akamrudisha.

²⁶ Sasa mimi—mimi ni... nafikiri kwamba Mungu yeye yule ambaye yule Mtakatifu mashuhuri Paulo alimwakilisha katika siku zake, kwamba alipohubiri kwa muda mrefu usiku mmoja, kisha mtu fulani akaanguka akaaga dunia; ndipo Paulo, alipomwendea yule mtu, kwa neema ya Mungu, aliwaambia makutano, “Uhai wake umo ndani yake.” Na—nafikiri kwamba inathibitisha kwetu, au kama kamwe hujalionga hapo awali, kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele.

²⁷ Pia yawezekana mambo yalikuwa hivi, kwamba nimejaribu kulifikiria adhuhuri hii. Kwamba, nimesimama hapa, na kwa moyo wangu wote nimewaambia Kweli kabisa, na kuwaambia kuhusu kinyongo changu, kisha nikakiri waziwazi, sababu... na kuwaomba muombe kwamba utu wangu wa ndani utabadilishwa kuwahusu watu, nipate kufanya kama Bwana alivyotenda. Na kuthibitisha kwamba Yeye bado atanipeleka kazini, Yeye aliachilia hilo litukie kuonyesha kwamba Yeye bado huponya wagonjwa na angeweza kufufua wafu. Basi nafikiri ilikuwa tu uthibitisho wa yale nilikuwa nikihubiri, na ambayo

nimekuwa nikishuhudia kuhusu Ufalme wa Mungu. Na hilo ni jambo la jinsi ile ile ambalo ndio kwanza Yeye amwambie Ndugu Roberson kule, na mwingine wa hao ndugu. Sasa twampenda Yeye kwa ajili ya hilo.

²⁸ Nasi tunashukuru usiku wa leo kwamba Ndugu Way yu pamoja nasi usiku wa leo. Na hakika Mungu hajamaliza na ndugu yetu, la sivyo angaliaga dunia asubuhi ya leo. Kuna kazi atakayofanya Ndugu Way. Nami nakutaka ujue, Ndugu Way, kwamba kanisa hili lote, pamoja na mimi mwenyewe, tutaomba kwamba Mungu atakuonyesha mpango Wake kwa maisha yako na ya mkeo; na mara ukiwa dhahiri, atakuweka humo. Nina hakika Yeye atalitekeleza, Ndugu Way. Na sisi sote, kama Wakristo, tutashukuru kwa ajili ya Ndugu Way. Hilo ni kweli, kanisa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Na tutaomba kwamba yeye pamoja na Dada Way watapata mahali pao katika Bwana, kwa utumishi wao maishani.

²⁹ Sasa, pia, nilitaka kuzungumza na Ndugu Way. Nimekuja mapema ili niweze kuzungumza naye na kutaka kujua maoni yake, au nini kilitukia. Naye hajui. Unaona, ulikoma tu, naye akaanguka tu na kuaga dunia. Hilo tu.

Ndugu Way, alikuwa anataka na akauliza kama kuna mtu ye yote katika jengo hili ambaye anashuka kwenda Arkansas, Jumanne ama wakati wo wote unaokwenda, kwe—kwenye mkutano huu. Sasa, la—labda ni mkutano mdogo sana. Ni undugu unakutana. Nami nafikiri ni huko juu mahali fulani porini, au mahali po pote pale, huko juu. Na pengine hakutakuwa na watu wengi sana, na—nadhani, mkutanoni, kwa sababu, kwa kweli, hata hawajui ninakuja, bado. Unaona? Na kwa hiyo marafiki wangu huko, itachukua siku moja au mbili usiku kabla hawajajua, hata marafiki wangu huko Arkansas, ambao wananjua huko, watakuwepo mkutanoni. Bali kama kuna mtu anayekwenda, na wangukuwa na nafasi kumbeba mtu mwingine, Ndugu Way angefurahi kufanya hivyo. Alisema itangazwe kuwa asingekuwa mzigo kwa watu, kwa kumtunza atakapokuwa huko, kwa sababu angeweza kujitegemea. Lakini yeye, kama kuna mtu anayeenda, ingekuwa ishara kwake kwamba Mungu angetaka yeye aende, au angekuwa katika—angekuwa katika mapenzi ya Mungu akishuka aende huko. Kwa hiyo ninyi nyote mnamjua Ndugu Way, ameketi hapa pembeni. Na ingawa mtu ye yote angetaka kumbeba, ambaye anaenda huko, na ana nafasi kwa abiria mmoja zaidi, yeye angefurahi kufanya hivyo.

³⁰ Basi usiku wa Jumapili ijayo, Bwana akipenda, nita—nitarudi, au asubuhi ya Jumapili ijayo, hasa. Na—na kama Ndugu Neville anaendesha shule ya Jumapili, na itakapomalizika, nataka kurekodi kanda nyingine nikiweza. Na kama sikukosea, nafikiri nitazungumzia juu ya *Maisha Yako* . . . *Je, Maisha Yako Yanaistahili Injili?* Kwamba, yaani, au,

Je mke Wako . . . Maisha Yanaistahili Injili? Hilo ndilo ninalotaka kusema. *Je, Maisha Yako Yanaistahili Injili?* Nami nataka kurekodi kanda juu ya hilo, Bwana akipenda.

³¹ Na sasa, usiku wa leo, nimetangaza kwamba leo nitarekodi kanda hiyo. Na mchungaji, hata sidhani alihubiri; aliniita tu, kuzungumza hapa jukwaani. Sasa, basi mimi sijui . . . Sasa, iwapo wao wanarekodi kanda, kama unaona unaelekea kuchoka au cho chote kile, unataka kutoka nje, hebu uwe kimya uwezavyo, kwa sababu hatutaki . . . Unaona, hizi—hizi maikrofoni ni nyepesi sana, sana kwa kunasa, na zinanasa kelele ndogo sana. Nasi tunarekodi, tunajaribu kurekodi kanda hizi kwa ajili ya huduma ya dunia nzima.

³² Na usiku wa leo nataka kutangaza somo langu kama lile . . . baada ya mimi—mimi kusoma Neno la Mungu, linalopatikana katika Injili ya Mathayo Mtakatifu, sura ya 24. Katika Injili ya Mathayo Mtakatifu, sura ya 24, basi na tuanze sasa kwenye aya ya 32 na tusome Maandiko.

Basi kwa mtini jifunzeni mfano; tawi lake likiisha ku—kuchipuka, na kuchanua majani, mwatambua ya kuwa wakati wa mavuno u karibu.

Nanyi kadhalika, myaonapo hayo yote, tambueni ya kuwa yu karibu, mlangoni.

Amini, nawaambieni, Kizazi hiki hakitapita, hata hayo yote yatakapotimia.

Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe.

Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, ila Baba peke yake.

Kwa maana kama vile ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu.

³³ Sasa katika somo letu, tunaona usiku wa leo, tunaposoma, kwamba sehemu ya kwanza ya sura hii inasema kwamba wanafunzi walimwita Yeye kando ya mlima, mlimani, wakamwambia, “Dalili ya mwisho wa dunia itakuwa nini? Nayo ni nini dalili ya Kuja Kwako? Na ni lini utakuja wakati ambapo halitasalia jiwe juu ya jiwe, kwenye hekalu?” Sasa anaendelea kujibu. Angalia hapa kwenye mstari wa 1.

. . . Yesu akaenda zake, akatoka hekaluni; wanafunzi wake wakamwendea . . . ili kumwonyesha jengo, la hekalu.

Naye Yesu akajibu akawaambia, Hamyaoni haya yote? Amini, nawaambieni, Halitasalia hapa jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomoshwa.

Na wanafunzi Wake... *Hata alipokuwa ameketi katika mlima...* (samahani)... *alipokuwa ameketi katika Mlima wa Mizeituni, wanafunzi wake wakamwendea kwa faragha, wakisema, Tuambie, mambo haya yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia?*

³⁴ Unaona, waliuliza maswali matatu, Naye anajibu maswali matatu. “Ni lini utakuja wakati ambao halitasalia jiwe juu ya jiwe? Ni nini dalili ya Kuja Kwako? Na vipi kuhusu mwisho wa dunia?” Na wengi, naamini, kwamba sisi ndugu tunafanya makosa kwa kujaribu kuliweka lote kwenye Kuja Kwake. Lakini Yeye anajibu maswali matatu mbalimbali aliyoulizwa. “Kwa nini kungekuwa na wakati ambapo halitasalia moja la mawe haya juu ya lingine; jambo hili litatukia lini? Nayo ni nini dalili ya Kuja Kwako? Na itakuwaje katika mwisho wa dunia?” Unaona, maswali matatu mbalimbali. Naye anaanza kwa kujibu moja, kuhusu lini “mawe yangeachwa bila moja juu ya lingine.” Ndipo baada ya Yeye kumaliza swali hilo, basi Yeye anaanza na, “dalili ya Kuja Kwake.” Ndipo basi anaingilia, “mwisho wa dunia.”

³⁵ Sasa tunaona hapa moja ya mambo ambayo nataka kuyazungumzia usiku wa leo, ni kile... *Kimulimuli Chekundu Cha Dalili Ya Kuja Kwake*. Nasi tunazungumzia usiku wa leo juu ya siku za Nuhu, “Ndivyo kutakavyokuwa kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Na sasa hili lilinijia mimi juzijuzi, nami nafikiri labda ningejaribu kurekodi huu kwenye kanda na kuzungumzia juu yake. Ndipo nikiandika Maandiko kadha hapa ambayo ningetaka kuyarejea, labda, na—na kuyasoma, katika muda kidogo.

³⁶ Lakini sasa Bwana wetu Yesu Kristo aliulizwa swali hili, Naye akawapa dalili ya Kuja Kwake. Na mara Yeye akasema hivi, “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita.” Halafu Yeye akasema, “Jifunzeni mfano wa mtini. Matawi yake yakiisha kuchipuka, mwatambua ya kuwa wakati wa mavuno u karibu. Kwa hiyo myaonapo mambo haya yakitimia, au yakidhihirishwa, jueni kwamba wakati umekaribia. Na kizazi hiki hakitapita hata mambo hayo yote yatakapotimia.” Kizazi kipi? Kizazi kile ambacho kitaona ule ukengefu tutakaozungumzia usiku wa leo.

³⁷ Kwa hiyo tufikiriapo kuhusu kifungu changu cha maneno, kama Kimulimuli Chekundu Cha Kuja Kwake, inanikumbusha kungojea kwenye stesheni ya gari la moshi, kwamba wakati mtu au watu wanaposimama hapo karibu, kama vile wengi wetu tumekwisha fanya, tulipokuwa tunangojea kupanda gari moshi. Na hatuwezi kusikia gari moshi, au hulioni, bali unajua wa—wakati umewadia. Pengine steshenimasta anasema, “Limechelewa ki—kidogo. Limechelewa kidogo, bali hatujui ni wakati gani, lakini litawasili hivi karibuni.” Nasi tutatembea—

tembea hapo stesheni, mikono yetu mifukoni, na kuketi juu ya makasha yetu, kisha kuamka kwenda kununua kifurushi cha njugu karanga, na kuzungumza na...mtu aliye upande wa pili wa barabara. Lakini mara tu tunaona kitu kikitukia. Kuna makelele yanayosikika nje kwenye reli. Na tulipoona, selo inashuka, ndipo kimulimuli chekundu kinaanza kumemetesha. Ni kitu gani? Gari moshi liko jengoni. Ingawa huwezi kulisikia, ingawa huwezi kuliona, hata hivyo kimulimuli hicho chekundu na kuteremshwa kwa ile selo kunaonyesha kwamba linakuja. Ndipo basi iwapo unatarajia kuondoka kwa gari mosho hilo, afadhali utupe chini kifurushi hicho cha njugu karanga, uache kupiga domo, uchukue makasha yako, ukajitayarisha la sivyo utaachwa, sababu litasimama hapo kwa muda mfupi tu. Litaondoka. Iwapo bado ungali umesimama ukipiga domo, yule jirani upande wa pili wa barabara, utaachwa.

³⁸ Ni zaidi vipi, basi, tuonapo selo ya kimulimuli kwamba Yeye yuko jengoni anakuja! Gari moshi la Injili ya zamani linapita, liko karibu sana. Na tunapojifunza usiku wa leo kuhusu kifungu hiki muhimu, dalili ya kimulimuli, kama Bwana wetu alivyoketi juu ya mlima na kuwaambia mambo haya yangetukia, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, hivyo ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.”

³⁹ Sasa tunataka kurudi nyuma, kwa kifungu kidogo, na kuona iwapo tunaweza kuona kitu cho chote katika siku hii ambacho kinafanana na siku za Nuhu. Ndipo tunaweza kujua basi mahali tulipo katika siku hiyo ambayo Bwana wetu alizungumzia, kuona kama iwapo twaweza kuona ulinganifu wo wote na siku za Nuhu. Ili kulitenda jambo hili, nafikiri yatubidi kurudi nyuma katika Kitabu cha Mwanzo, kwenye siku za Nuhu. Na kama mtafungua pamoja nami, tafadhalini, katika Maandiko, nyuma katika Mwanzo sura ya 6, na hizo ni siku za gharika, na uadilifu na hali za siku ile, Mwanzo sura ya 6. Sasa, tunataka kusoma, angalia na ulinganishe siku ile na siku hii. Tazama.

Ikawa wanadamu walipoanza kuzidi usoni mwa nchi...

⁴⁰ Neno la kwanza kabisa latuonyesha kimulimuli halisi kwamba ile siku imekaribia, kwa maana hakujawahi kuwa na wakati katika historia yote ambapo kumekuwa na watu wengi hivyo, na wanaoongezeka haraka sana, kama tulio nao leo, hata ni vigumu kupata mahali pa kuishi. Basi kuna ongezeko kubwa sana la watu juu ya uso wa nchi, mpaka sayansi inasema, kwamba, “Ikiwa wataendelea kuongezeka kama wanavyofanya, mnamo miaka ishirini hata hakutakuwa na chakula duniani cha kuwatosha watu.” *Readers Digest*, naamini ndilo, ambalo lilinukuu jambo hilo, kwamba, “Hata hakutakuwa na chakula cha kuwatosha watu ambao wanaongezeka haraka sana.”

41 Tunaweza kuangalia kila mahali na kuona kwamba sehemu zilizokuwa nyika zimegeuka jiji, hata ingawa upangaji wa uzazi umetia fora sana kuliko ilivyopata kuwa. Naamini ilinenwa kuhusu Chicago... Natumaini sinukuu takwimu hizi vibaya. Bali kwa kweli visa vilivyoorodheshwa, visa thelathini elfu vya kutoa mimba kila siku sitini, huko Chicago. Visa vya kutoa mimba kila siku sitini, vilivyoorodheshwa! Vipi kuhusu hivyo visivyoorodheshwa kamwe? Unaona, katika jiji moja kubwa tu la watu milioni nne! Vipi kuhusu ulimwengu? Na bado watu wamesongamana hata hawawezi kuwashughulikia...

42 India, wanajaribu kuwa... kukatiza sehemu ya kibinadamu ya mwanamume, na kuwafanya towashi, ili watoto wasizaliwe, kwa sababu wana—wanaongezeka sana. Milioni mia nne na sabini, wakati huu, huko India.

43 Vipi kuhusu China, ambako ongezeko ni kubwa zaidi, Urusi na nchi zingine za ulimwengu? “Watu walipoanza kuongezeka juu ya uso wa dunia.” Unaona? Sasa tunarudi kwenye wakati wa gharika.

...wana wa kike walizaliwa kwao. Wana wa Mungu waliwaona hao binti za mwanadamu ya kuwa ni wazuri; wakajitwalia hao wake...wo wote waliowachagua.

BWANA akasema, Roho yangu haitashindana na mwanadamu milele, kwa kuwa yeye naye ni nyama; bali siku zake zitakuwa mi—miaka mia na ishirini.

Nao Wanefili walikuwako nchini siku zile; tena, baada yao...wana wa Mungu walipoingia kwa binti za mwanadamu, wakazaa nao wana; hao ndio walikuwa wanadamu hodari zamani. watu wenye sifa.

44 Loo, ni so—somo jinsi gani tulilopata hapa! Unaona? Sasa, moja ya mambo ya kwanza ninayotaka uone, kwamba wa—wana wa Mungu waliwaona binti za wanadamu, kwamba walikuwa wazuri. Sasa si... Ninalielekeza hili ulimwengu mzima. Lakini hapajawahi kuwa na wakati duniani, kadiri ninavyoweza kuwaza, ni wakati ule tu, ambapo kuliwahi kuwa na—na urembo wa jumla miongoni mwa wanawake.

45 Basi mnaweza kukumbuka, baadhi yenu enyi wanawake wazee, na baadhi yenu watu, wanaume, ambao mnaweza kukumbuka huko nyuma miaka mingi iliyopita, jinsi ilivyokuwa shida kumpata mwanamke mrembo. Bali leo huoni ye yote isipokuwa aliye mrembo. Ni kwa sababu kwamba wamefikia mambo haya yote ya kukata nywele zao, na kujipodaa, na—na aina zote za nguo za kutamanisha na kadhalika. Wanaweza kujitoa wenyewe kwa njia hiyo. Na sasa ni, jambo jingine, mkono wa saa umerudi nyuma, kulingana na Maandiko. Na wanawake daima wanazidi kuwa warembo.

⁴⁶ Naweza kukumbuka nilipokuwa mvulana mdogo shuleni, nami ninageuka kuwaangalia watoto wadogo siku hizi, wasichana wadogo wanaokua. Nami naweza kutazama, kufikiria juu ya wanawake nilipokuwa kijana mwanamume, na kuwaangalia wasichana siku hizi. Nakumbuka kungekuwa na msichana mmoja anayependwa na watu wengi, na hiyo haizidi miaka ishirini na mitano iliyopita, msichana mmoja anayependwa na watu wengi, msichana mrembo, na karibu kila mvulana alitaka kumwadama msichana huyu, kwa sababu yeye alikuwa malkia wa—wa kundi. Pengine katika mji mzima, kungekuwa na wawili ama watatu wa hao wanawake. Sasa wote wamekuwa warembo, wote. Hilo ni kutimiza Maandiko, na kimulimuli chekundu kwamba wakati umekaribia.

⁴⁷ Wamebuni vitu kama rangi ya midomo na—na vipodozi, hata mwanamke ambaye si mrembo sana, bado anaweza kujifanya mrembo kwa yale—vipodozi vyote vya kurembesha uso na ma—mambo wanayofanya kujirembesha.

⁴⁸ Max Factor inafanya kazi mchana na usiku, na kuna fedha nyingi zaidi zinazotumiwa kwa vipodozi, Marekani, katika mwaka mmoja, kuwarembesha wanawake, kuliko zinazotumiwa katika maduka ya vyakula. Hiyo ni kweli, ninasahau ni dola bilioni ngapi kila mwaka zinazotumika kwa vipodozi, kuwarembesha wanawake wetu.

⁴⁹ Sasa sisemi cho chote kupinga hilo, ninawaonyesha tu kwamba ni kimulimuli chekundu kwamba wakati umekaribia. Kwani Yesu alisema, Mwenyewe, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Unaona, jambo lile lile.

⁵⁰ Pia angalia, “Watu walipoanza kuongezeka, watu wengi. Binti za wanadamu walikuwa wazuri; na wana wa Mungu waliwaangalia, nao wakajitwalia wake.” Sasa, huo si usemi wangu binafsi. Ninalisoma katika Biblia, ambapo Yesu alituambia turudi katika Mwanzo na kulinganisha siku hizi pamoja. Ongezeko la watu, na urembo wa wanawake, sasa hiyo ni ishara kubwa.

⁵¹ Sasa onyo, onyo la Yehova, aya ya 3.

BWANA akasema, . . .

⁵² Mara baada ya jambo hili kutukia . . . Kumbuka, Roho Mtakatifu aliandika Biblia, na Yesu alipewa nguvu na utimilifu wa Roho Mtakatifu. Naye alinena tu kwa Roho Mtakatifu. Na Maandiko yameandikwa na Roho Mtakatifu. Na Yeye yule hasa aliyeandika Mwanzo 6, alituambia katika Mathayo 24, tukijua wakati umekaribia, turejee katika Mwanzo 6 na kulinganisha na hayo.

⁵³ Ongezeko la watu duniani; na hata hivyo upangaji wa uzazi, na hayo mambo yote yanayotendeka, hata haulipunguzi.

Linatendeka hata hivyo, kwa sababu tuko katika wakati wa mwisho.

⁵⁴ Basi angalia, mara kukaja wakati iliposemwa wanawake walikuwa warembo sana, wenye sura nzuri sana. Nasi tukilinganisha hilo kwa hili twaweza kulihakikisha.

⁵⁵ Sasa, nilikuwa nikiangalia picha za wakati mrefu uliopita wakati babu zetu, walipovuka zile nyanda. Na siwezi kukumbuka ji—jina la yule mwanamke, lakini jina lake lilijulikana toka San Francisco hadi—hadi Boston, kwamba ndiye alikuwa mwanamke mrembo zaidi nchini. Pearl White, naamini, ndilo jina lake, wa miaka mingi iliyopita. Alivawa na mpenzi wake, Scott Jackson. Na kama ungeiona picha ya huyo mwanamke, ati ndiye bibi mrembo zaidi ya wote nchini, ingekuwa vigumu kwako kumwangukia. Angeonekana kama kitu cha kale hapa nje barabarani. Kwani, karibu mwanamke ye yote ambaye ungemwangukia kwa namna yo yote upendavyo, angekuwa mrembo mara tatu zaidi yake, mwanamke ye yote leo ambaye ungemwona akipita barabarani. Unaona, ni kuongezeka, urembo wa mwanamke.

⁵⁶ Na halafu ninashangaa kama wanawake wetu wanatambua hili na wanaweza...Hiyo ndiyo sababu nataka kanda hii iende, ili—ili usiweke sana...Tunataka muwe wenye sura nzuri, lakini tunataka muwe wa kawaida. Hatutaki muwe wa kijuujuu. Baadhi ya wanawake hawa warembo, kama ungewachovya kwenye pipa la kuvulia muda kidogo na kuwaosha, wangeonekana tofauti kidogo, na—na kuwavalisha jinsi iwapasavyo kuvaa. Lakini wao—wao—wao hawafanyi hivyo, wala huwezi kuwaambia vinginevyo. Na tutalifikia hilo baada ya muda kidogo. Lakini ni kile—kile kimulimuli chekundu.

⁵⁷ Pia kumbuka, watu walipoanza kuongezeka juu ya nchi, na wanawake wakawa warembo, ni saa hiyo, ilikuwa wakati huo ambapo:

...BWANA akasema, Roho yangu haitashindana na wanadamu...

Unaona ule mfumbato? Unaona mkono wa Mungu? “Roho Yangu”...Binti za wanadamu walikuwa warembo, nao wakajitwalia wake. Naye akasema, basi “Roho Yangu haitashindana na mwanadamu milele. Nitazifupisha siku zake.”

Sasa aya ya 4:

Nao Wanefili walikuwako duniani siku zile; tena, baada ya hayo,...wana wa Mungu walipoingia... kwa binti za wanadamu, au—au binti za mwanadamu, wakazaa nao wa—wana, na hao ndio watu waliokuwa hodari zamani...watu wenye sifa.

⁵⁸ Umechunguza haikusema neno kamwe kuhusu ndoa? Angalia, “Wana wa Mungu wakaingia kwa binti za wanadamu,” hakuna neno kuhusu ndoa. Na kama ukilichukua katika Kiyunani cha asili hapo, maana ya neno hilo, kinasema, nimeliandika hapa mahali fulani, “mke.” Walijitwalia “wake,” katika aya ya 3, “walijitwalia wake.” Katika Kiyunani, niliangalia adhuhuri ya leo, halikusema, “Walijitwalia wake.” Lilisema “Walijitwalia wanawake,” sio wake. Sasa hebu lithibitishe hilo na—na... Emphatic Diaglott, uone kama hiyo si kweli.

⁵⁹ “Walijitwalia wanawake,” sio wake. Walijitwalia tu kama walivyokuwa, wapenzi wa holela, kama vile ilivyo leo. Maneno mengine, walikuwa vimada siku hizo kama tu walivyo leo. Walishika njia yo yote waliyotaka, na kujitwalia mwanamke ye yote waliyeweza.

⁶⁰ “Na wakati wana wa Mungu...” Sasa, wengi wao husema hapa kwamba hao walikuwa ni Malaika walioanguka, na kadhalika, na hao wanaume na wanawake. Lakini kuonyesha ya kwamba ni kosa, ni kosa kabisa, Biblia haisemi mahali po pote kuhusu Malaika kuwa aidha wanaume au wanawake. Na, isitoshe, hakuna mwa—mwanamke aliyetajwa kuwa ni Malaika, katika Biblia, kamwe. Sasa kama unataka Maandiko juu ya jambo hilo, Mathayo 22:20, na kadhalika, unaweza kulipata.

⁶¹ Sasa, hilo, hilo, hakuna kitu kama malaika mwanamke. Hiyo ndiyo sababu kwamba mhubiri mwanamke... *Malaika* ni “mjumbe.” Na ni—na ni... *malaika* ni “mjumbe.” Na hakuna kitu kama hicho. Bali, unaona, wamebadilisha, leo, kama ilivyokuwa siku hizo. Sasa, nina mambo yaliyoandikwa hapa ya kihistoria, tunataka kuyafikia katika dakika chache.

⁶² Angalia, wanawake wa siku ile, katika siku za Nuhu, lazima walikuwa ndio maongezi ya siku ile. Unaona, “wana wa Mungu,” wa Sethi, wana wa Sethi, waliwaona binti za Kaini, kwamba walikuwa warembo. Kwa nini? Walikuwa waovu, nao walikuwa binti za Kaini. “Wana wa Mungu walipowaona binti za wanadamu, walikuwa warembo, wakajitwalia wanawake.” Ndipo wana wa Mungu walipoanguka kutoka cheo chao na Mungu, na wakawa wenye kuadama wanawake.” Na kama hivyo sivyo mambo yalivyo leo hii, sijui yalivyo. Hiyo ni kweli.

⁶³ Mwanamume! Hata angalia makanisa yetu leo, angalia kila kitu unachotaka kuangalia, chunguza jambo hilo. Kila mahali, ilionekana katika siku ile, lazima walikuwa wanawake wazuri. Wanaume walikuwa watumwa kwao, historia inasema, kwamba wanaume kwa kweli walikuwa watumwa wa wanawake, kwa sababu walikuwa warembo sana, hata wakawa watumwa. Kwa kweli waliwatengenezea madhabahu, wakawaabudu. Na, hebu wazia, kwa kweli waliabudu mwili na damu ya mwanamke zamani zile. Hiyo ni historia.

⁶⁴ Basi linganisha hilo na leo. Ni kitu kile kile, ndugu yangu. Wanaume kwa kweli wanawaabudu wanawake. Mbona, katika nchi yetu wenyewe, Bibi Kennedy anafikiriwa mara mbili zaidi, kuliko ilivyo kwa Rais. Hiyo ni kweli. Na iwapo sikuzote unazungumza kuhusu mwanamume, kama ana mwanamke anayevutia, haya basi.

⁶⁵ Na sasa wanasema hivyo kuhusu kuendesha magari. Unawasikia wakisema wanawake ndio madereva walio bora sana. Sivyo, kwa sababu nitawaambia kwa nini. Mimi na Billy, tukisafiri kote Marekani, tukijionea wenyewe, tuliweka ramani ndogo katika ninino, kijibao kidogo cha kuandikia, tukaandika “mwanamume” na “mwanamke.” Na kila wakati mwanamke alipokosea, tuliweka alama upande wake; na mwanamume alipofanya kosa, tungeweka upande wake. Na katika mia tatu, tunaoita “zomea,” wamewekwa kando ya barabara, ungelishangaa. Kulikuwa na wanawake mia mbili na themanini, ukilinganisha na wanaume kumi na tisa. Lakini unajua kwa nini? Hawapeleki hilo kwenye mahakama za polisi. Polisi hatamshika msichana mrembo; mmoja katika elfu moja. Kweli, atachukua namba yake ya simu, bali hatamkamata. Na hivyo ndivyo ilivyo. Si ajabu rekodi hazilionyeshi. Unaona? Kwa sababu, wanaume leo wako kama walivyokuwa katika siku za Nuhu, wanasujudia madhabahu ya wanawake warembo. Hiyo ni kweli. Loo, jamani!

⁶⁶ Jinsi hapana budi ilikuwa baya sana siku hizo, jinsi walivyoabudu, hao wanawake, wakiiacha miili yao hivyo wapate kutamanisha. Na kama walikuwa hodari zaidi kwa kufanya jambo hilo, kuliko walivyo siku hizi, nafurahi sikuishi wakati huo. Hebu lifikirie jambo hilo, jinsi ambavyo wao tu... jinsi ambavyo wanawake wameanza kutenda wanavyotenda sasa.

⁶⁷ Angalia, Biblia ilisema, “Walikula na wakanywa.” Sasa, hilo—hilo ni halali. Hakika.

“Ndoa ni ya kuheshimiwa.” Mwanamume, mwanamume anamuoa mwanamke, hilo ni jambo la heshima, hilo lilianzishwa na Mungu. Bali inapokuja wakati mwanamume atamchukua mke wa mtu mwingine, au amtwae kijana mwanamke, au mwanamke fulani haidhuru yeye ni nani, avunje nadhiri yake ya ndoa, na kufanya jambo ambalo si halali, ni dhambi mbele za Mungu. Na Biblia inazungumzia jambo hilo na kulipinga kwa ukali sana.

⁶⁸ Sasa angalia, Hiyo inasema hivyo. Ndoa, Mungu aliianzisha hiyo huko Edeni, bali Yeye hakika alilaani uzinzi. Na wanaume hawa na wanawake, katika siku ile, walikiuka amri za Mungu, na wakajiamulia wenyewe na kulitenda, kwa vyo vyote. Sasa, linganisha jambo hilo na leo. Liangalie. Kama ukitaka kuona kwamba gari moshi tayari limefika, hebu wazia hilo kindani

sana sasa, kwa kuwa Yesu Kristo asiyekosea ndiye aliyesema Maneno haya. Unaona?

⁶⁹ Basi angalia, Biblia ilisema hapa, “Walikula na wakanywa,” bila shaka, pamoja na wanawake warembo. Sasa, tunatambua kwamba hilo ni sawa. Kula na kunywa, hizo ni moja za kawaida za maisha. Hatuna budi kufanya hivyo. Bali ikiwa hilo ndilo linalojaza akili yako, leo hii watu wamekuwa walafi, walevi, wanawake wakinywa pombe hotelini. Na ulienda mahali ambapo po—pombe kali na vinywaji vikali sana vinaandaliwa, wanawake wanakunywa zaidi ya wanaume.

⁷⁰ Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, walikuwa wakila, na kunywa, na kuolewa.” Kwa maneno mengine, walikuwa wakiishi na wanawake bila ya kuwaoa. Na leo, mbona, imekuwa desturi kabisa. Walikuwa na Reno, ambapo ungeweza kuoa, na kutaliki na kuoa tena, yote katika siku moja. Lakini tendo hilo sasa ni la kizamani. Hao—hao waume, kama wajiitavyo, na hao wake, hubeba funguo mbalimbali za vyumba kwenye miji hii mikubwa. Sasa, mimi husafiri. Na—naishi katika miji mikubwa na najua hilo ni kweli, kwamba mume ana miadi yake, na mke ana miadi yake. Naam, ni kusanyiko la uvundo hivi kwamba, hata imezaa kundi la—la kizazi teketeke, kivivu, kisichofaa, kinachoelekea jehanum.

⁷¹ Miaka michache iliyopita, angalia ambapo binadamu amefikia, katika mwili wake. Angalia alipofikia, kwa mambo aliyotenda. Sayansi daima inajaribu kutengeneza chakula bora zaidi, mahindi ya kisasa, na—na nyanya za kisasa, nyama za kisasa, na huku chakula hicho hakifai kabisa. Kinaua watu, nao hawatambui. Mbona, mnamo miaka michache ijayo, hawatakuwa kitu ila ku—kundi la watu yavuyavu.

⁷² Miaka hamsini iliyopita, michezo ya kandanda iliendelea kama ilivyo siku hizi, wala hukusikia kamwe mtu ye yote aliyeumia, bali sasa inaua dazani moja, au mbili, kwa mwaka. Mpira utampiga mtu, yeye, hana cho chote ndani yake cha kushikilia uhai wake mle ndani. Yeye yuko kama sili. Unampiga, ni teketeke sana, amekwisha kufa.

⁷³ Wakati Bob Fitzsimmons alipopigana na Corbett, naamini walipigana raundi mia moja ishirini na tano, aduhuri moja, mikono mitupu. Wakati watu hao kwa ngumi hiyo ya mikono yao wangepiga kuchukua mbili kwa nne, kwenye nchi nne, na kuponda ile mbili kwa nne bila kitu ila ngumi kavu tu. Walilala wameichovya mikono yao katika siki, kuzifanya ngumi zao ziwe ngumu. Na ra—raundi haikuwa ndogo ya dakika mbili tatu kama tulizo nazo leo. Hawakuwa wamevaa glavu zenye manyoya mikononi mwao, na hakuna mtu aliyeuawa. Nao wakapigana. Raundi ilikuwa ni kumbwaga chini. Ilikubidi umwangukwa mtu chini. Nao walipigana mara mia moja na ishirini na tano wakibwaga chini. Hao walikuwa wanaume. Na leo itawabidi

wakomeshe mashindano ya ndondi, na huku wanavaa glavu zenye manyoya laini mikononi mwao na katika makonde yao, hawawezi kupigana raundi mbili au tatu bila ya mtu kuuawa. Kuna nini? Amefanywa kwa tita la, sijui, takataka nyororo, mchanganyiko mtupu, mpaka kizazi chote kinakufa.

⁷⁴ Hivi Biblia haikusema hilo, kwamba wangekuwa dhaifu zaidi na werevu zaidi? Mbona, jamii ijayo ya wanadamu, wataishi kwa kidonge, watakula kidonge kwa chakula chao cha kutwa. Si kitu ila kundi la watu wenye kuvuta sigara, kunywa wiske, wanaokimbilia vinywaji vikali, kundi lililoharibiwa na madawa ya kulevya, na ya kujidunga sindano. Matineja shuleni, na uvunjaji sheria wa watoto, si ajabu, mama yake akiwa huko barabarani, akitenda jinsi anavyotenda, inamtumbukiza mtoto kwenye jambo lile lile.

⁷⁵ Ongezeko la wanawake warembo; maisha ya umma yamevurugika. Loo, jamani, ni jambo kuu jinsi gani katika siku tunayoishi! Jinsi wanavyolitenda hili, ni... kuchukuliana na hilo. Hawataepuka. Wanafanya nini? Kama tu walivyotenda wakati huo, wanadhihaki Amri za Mungu. Mungu alisema, "Usizini." Lakini wanaonyesha kwamba wanaweza kulitenda, na kuepuka. Wanafikiri wataepuka, bali hawataweza kamwe. Labda hupaswi kuja, kusikiliza haya. Ha? Hata hivyo, Mungu alisema kwamba huu ndio wakati ambao kimulimuli chekundu kingememetesha. Yesu alisema hivyo.

⁷⁶ Sasa ni—ni dhambi ya jinsi gani wanayotenda, na kuchekelea dhambi! Mara nyingi, hiyo, jambo lile lile ambalo Biblia hii inaliita ufisadi, ulimwengu leo unaliita jema. Unapowachukua wasichana wadogo, na kuwavua nguo zao, na kuwaweka nje huko huku wamevaa kaptura, wamevaa suruali, na kadhalika, na kutembea barabarani, nao wanafikiri ni sawa kwa msichana kuonyesha mwili wake wa kike. Ambapo, Biblia inasema ni dhambi, ni chukizo! Lakini ulimwengu huliita jema. Unaona, wanafanya Amri za Mungu... Na kanisa halisemi neno juu yake. Wakati umewadia ambapo mtu fulani anapaswa kusimama katika jina la haki, katika Jina la Yesu Kristo, na kulikomesha jambo hili, sababu siku moja tutawajibishwa jambo hilo Siku ya Hukumu.

⁷⁷ Naam, kama hili likisikika la kale na la kijinga, kwa mtu fulani, chunguza miaka michache kule nyuma halafu uone yanayotendeka sasa, halafu uwazie ya usoni. Hakuna ya usoni ila Kuja kwa Bwana.

⁷⁸ Angalia, linganisha wanawake hawa wa nyakati zilizotangulia gharika na yanayotendeka leo; chunguza walivyokuwa. Chunguza walivyotenda wana wa Mungu; chunguza wanavyotenda leo.

⁷⁹ Nilikuwa nimeketi mkutanoni si muda mrefu uliopita, na karibu nizimie, wakati hao wote... Ilionekana kama kila

mtu anafurahia mazungumzo ya muhudumu fulani, aliyekuwa amesimama jukwaani. Nami nilikuwa nimeketi pembeni. Basi akaja ki—kijana mwanamke, naye alikuwa amevalia vibaya sana. Naye akaja akitembea ndani ya kanisa hili, kama inavyosema Biblia, akienda kwa hatua za madaha. Na kila mhubiri jukwaani, pamoja na kusanyiko, kila mmoja akigeuza kichwa chake na kuangalia, wakimfuatilia msichana huyu. Nami nikafikiria Andiko hili, “Wana wa Mungu waliwaona binti za wanadamu,” wanawake warembo, wenye dhambi, wasiomcha Mungu. Loo, jambo hilo limeyavunja makanisa mengi vipande-vipande. Liliondoa Roho wa Mungu! Angalia, “Waliwaona binti za wanadamu.”

⁸⁰ Sasa kumbuka, Yesu Kristo asiyekosea alisema kwamba mambo haya yangukuwa hivi katika siku hii. Naye alisema, “Myaonapo mambo haya yakitimia, basi mnajua kwamba wakati upo mlangoni.” Sasa, hakuna watu wengi watakaosema hayo. Kuna wahubiri wengi ambao hawangesema hayo. Angeweza, kama angetaka. Lakini kama angesema, kusanyiko lingemfukuza. Hiyo ni kweli kabisa.

⁸¹ Lakini hapa pana jambo moja. Kama mtu ameitwa na Mungu, atadumu na Biblia hiyo, sijali ambalo litampasa kutenda. Yakubidi ukumbuke kwamba Hilo ni Kweli. Na Kweli hufunga au huweka huru. Na hivi ndivyo Yesu Kristo alisema hasa.

⁸² “Wana wa Mungu walianguka kwa sababu ya maumbo mazuri na nyuso, za binti za wanadamu.” Na hilo ndilo tulilo nalo hasa leo hii, jambo lile lile tena.

⁸³ Sasa, linganisha siku ile. Ongezeko la watu; wanawake wakizidi kuwa warembo; wana wa Mungu wakianguka; kuoa na kuolewa; kesi za talaka; kuishi katika uzinzi; na kadhalika.

⁸⁴ “Mbona” unasema, “Ndugu Branham, hebu kidogo. Sijui.”

Sikiliza, ndugu, kabla tu ya kusema kitu, sikiliza hili. Yesu Kristo alisema, kwamba, “Kila amtazamaye mwanamke akamtamani, amekwisha zini naye tayari moyoni mwake.” Na unapoona... Mtu anapotoka afisini mwake, anapotoka kanisani, anapotoka nyumbani kwake, akaingia barabarani, unaona nini ila onyesho, kila upande, la miili na damu ya wanawake, nguo zilizobana, uso mzuri, unajaribiwa. Hilo ndilo Mungu alisema lingetukia. Hilo litukiapo, basi wakati upo mlangoni.

“Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, wakati wana wa Mungu walipowaona binti za wanadamu, na wakaanza kujitwalia wanawake.” Unaona? Basi.

⁸⁵ Sasa angalia. Tunaona kwamba, jambo lile lile leo. Tunaona katika historia, kwamba walikuwa wanatamanisha sana, mpaka wana wa Mungu wakajitengenezea madhabahu za

wanawake. Kama vile ya Venus, na kadhalika. Unaona? Wao, walitengeneza madhabahu, kisha wakayasujudia. Unaposema, “Ndugu Branham, hatuna mambo kama hayo leo. Usingeweza kulinganisha zamani hizo na siku hizi.” Samahani. Naamini ni mbaya zaidi leo kuliko ilivyokuwa wakati huo.

⁸⁶ Tunaona nini? TV! Hata huwezi kuchukua gazeti bila kuona kila kitu unachoangalia kimejazwa wanawake. Wanawake warembo katika kila kasha la wiske, katika magazeti, wamevalia kizinifu na kivasherati. Kwenye TV, katika kila kitu, ni baadhi ya wanawake waliovalia kizinifu, wanawake warembo. Na tunaona kwe—kwenye matangazo ya sigara, kila kitu ambacho unaweza kuangalia, utaona kwamba ni mwanamke anayevutia. Hata huwezi kuona tangazo la soksi ndefu za hariiri mpaka uone namna fulani ya miguu myembamba imeingizwa ndani yake. Na hiyo ni kweli. Lakini ni nini? Mbona hivyo?

⁸⁷ Ninakumbuka mtu niliyefanya kazi kwake, Chris Meisner, juu hapa pembeni. Wengi wenu mnamkumbuka Chris Meisner. Mke wake, Lillian, jina lake lilikuwa Lily, nafikiri, Ellinger. Na wakati alipo. . . Mtu mmoja alimjia. Huyu alikuwa msichana mwenye sura nzuri. Na mtu fulani alitaka apate ruhusa toka kwa baba yake, kuweka uso wake, picha yake, sura yake, kwenye kasha la peremende. Na huyu mzee Mluteri wa Kijerumani akasimama kwa miguu yake, akasema, “Huko ni kunitusi mimi, kuweka picha ya binti yangu kwenye kasha la peremende, ikaenezwe nchini kote.” Na leo je? Wakati, vibao vya matangazo, televisheni, kila unachoangalia, ni wanawake waovu, wachafu, washerati, wasiomcha Mungu. Hilo ni kweli. Ni nini? Gari moshi, lile gari la kale—lile gari moshi la kale tayari limo jengoni sasa. Biblia ilisema hivyo, litakuja hivi karibuni. Tunasikia sauti yake.

⁸⁸ Tunazungumzia mambo mengine kuhusu jambo hilo, bali, kumbuka, hiki ni kimulimuli kingine, moja ya vimulimuli ambavyo vinamemetesha mbele yetu leo. Loo, tunaona hali ya taifa; tunaona vurugu za siasa; tunaona hali ya kanisa. Tunahubiri juu ya yote hayo. Bali hili ni jambo jipya. Ni jambo ambalo halipendwi kuzungumziwa sana na watu, bali lazima lifanywe, kwa maana yabidi kuwe na sauti inayolia. Kumbukeni, maneno yaya haya ninayonena usiku wa leo yatakutana nami huko ng’ambo kwenye Hukumu. Unaona?

⁸⁹ Nilipomwona mwanamke huyu si muda mrefu uliopita, kwenye ono alilonionyesha Bwana, nikamwona akifa. Huyu, siwezi kukumbuka jina la mwanamke yule, yeye, Marilyn Monroe. Nami sikuwa nimemwona hapo awali. Siendi kuona sinema. Bali nilikuwa ni—ni—nilikuwa nimemwona msichana yule, naye alikuwa anavutia. Naye alikuwa akijaribu kukifikia kitu fulani, alikuwa anakufa, alikuwa ana ugonjwa mbaya wa moyo. Ndipo Bwana akasema, “Sasa wewe useme kwamba, ‘Amefariki yapata saa kumi. Hakujiva.’” Kasema, “Lakini

unaweza kusema alikufa kwenye saa kumi, sababu ni saa kumi kasoro nukta chache.” Na hapo niliona mahali walipompata. Basi nilimwambia Billy, nikaiambia jamaa yangu, wale waliokuwa pamoja nami, kuhusu jambo hilo. Na siku chache baadaye, ikawa Marilyn Monroe ndiye aliyefariki.

⁹⁰ Sasa, nilipokuwa Canada juzijuzi, watoto wangu walizidi kuniambia, mahali fulani ambapo bibi fulani alitupangisha nyumba, alikuwa na televisheni. Nao wakasema, “Kutakuwa na mchezo wa kuigiza, uitwao, Mto Wa Kutokurudi.” Huo ndio mto ninakovua samaki, wakati wote. Na John Smith, rafiki yangu, ndiye anayefanya safari hiyo. Kasema, “Wamefanya sinema yake.” Wakasema, “Baba, pengine Bw. Smith yumo kwenye kipindi hicho. Ungetaka kukiona?”

“Vema,” nikasema, “nitakaporudi kutoka Canada, kama nikiwahi kwa wakati mzuri, nitakiona.” Vema, wakati mchezo ule ulipokuja, nikaenda kule kuuona, nikaenda kuuona. Ndipo nilipoenda, aliyekuwa akiucheza ni nani ila Marilyn Monroe. Sasa, huyo hapo, amekwisha kufa mwaka mmoja au zaidi, huyo hapo amevaa kivasherati kitupu. Hiyo hapo sauti yake, ingali inacheza; na itacheza, kwa miaka na miaka, kwenye hiyo kanda ya sumaku. Kama kanda hiyo ya sumaku ingeshikilia kitendo chake, ambapo kama angeweza kuangalia kutoka mahali alipo usiku wa leo . . . Natumaini ameokoka, lakini sijui; hilo ni juu ya Mungu. Bali kama angeweza kuangalia nyuma, hawezi kukana hilo. Hawezi kuikana hii, kwa sababu tunayo. Ni zaidi jinsi gani Mungu ana kila msogeo, kila kitendo, kwenye kanda Yake yenye uwezo mkuu sana ambayo itakuwepo. Hatuwezi kuikwepa. Ipo papo hapo.

⁹¹ Tena kumbukeni, kama kungekuwa na maikrofoni imekaa papa hapa ambapo *hili* lipo, na nilikuwa nikiutangazia ulimwengu sasa, watu wa ulimwenguni kote wangeisikia sauti yangu kabla hata haijavuka mimbara hii kuwafikieni ninyi. Hilo ni katika elektroniki za ulimwengu.

⁹² Na unajua, sauti hiyo haifi kamwe. Haitakufa kamwe. Sayansi inadai, “Katika miaka ishirini,” kama wanaweza kuendelea wanavyoendelea sasa, “Kwamba watanasa Sauti yenyewe ya Yesu Kristo wakati alipokuwa duniani, kwenye miaka ishirini tangu leo.” Kwa sababu, ni kama kuangusha changarawe kwenye kidimbwi, huenda mawimbi yake madogo hatimaye yakafifia usiyaone tena, bali sayansi inadai yanarudi kwenye ukingo mmoja, yakavuka bahari hadi ukingo wa pili, na kusogea huku na huko, na hayafi kamwe. Wala pia maneno unayonena; yatakutana nawe Siku ya Hukumu, nayo yatakuhukumu au yatakuokoa, na hatuwezi kamwe kukwepa jambo lolote.

⁹³ Nasi tunafahamu sana, picha za watu zinapita moja kwa moja katika chumba hiki sasa. Kama huamini hilo, fungulia televisheni. Na kuna sauti za watu, lakini hisi zetu hazitazihisi.

⁹⁴ Sasa, wana stesheni ya kutangazia na mtambo wa sumaku, au bomba, au kioo ambacho hunasa sauti hizo na kuzitoa tena. Na jambo pekee Biblia ilivyo, ni hili, Neno la Yesu Kristo ambalo Yeye alilinena, Nayo yanaishi kweli kama tu neno lingine lilivyo ulimwenguni usiku wa leo.

⁹⁵ Sasa, iwapo moyo wako tayari umesafishwa kwa Damu ya Yesu Kristo, na unakuwa chombo cha kupokea toka kwa Chombo kinachotuma, ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na anafanya mambo yale yale Yeye aliyofanya, sababu Neno Lake haliwezi kufa. Yanaishi milele. Haiwalazimu kuchukua chombo, au miaka ishirini tangu leo. Tunalipokea Hilo sasa hivi. Sasa, naam basi.

⁹⁶ Tukiishi katika siku hii maarufu ambayo tunaishi, inayokaribia kuja kwa Mwana wa Adamu, na taa zinamulika kila mahali, za Kuja Kwake. Tunaiona katika siasa, tunaiona katika kanisa; tunaiona katika siku hizi; tunaiona katika kila mahali tunapoiangalia. Tunaona jua halionekani kama lilivyokuwa hapo awali.

Ulimwengu umevurugika. Wananiambia sasa hivi, kwenye Ncha ya Kaskazini, mle ndani, kwamba bahari imekuwa, ninasahau kiasi gani, na kina kirefu kuliko ilivyokuwa. Mlangobahari wa Bering, ungaliweza kuuvuka kwa miguu. Sasa, kuna kina kirefu, sana, cha futi nyingi, kwenye Mlangobahari wa Bering. Kwa nini? Dunia inavimba katikati. Inakuwa na kina kifupi hapa ambapo ilikuwa na kina kirefu, na kuwa na kina kirefu hapa ambapo ilikuwa na kina kifupi. Ulimwengu umevurugika kabisa. Unabatabata. Unawayawaya. Maumbile ya asili yote yanaachilia, na kila kitu tunachoweza kuona.

⁹⁷ Na sasa, usiku wa leo, tunaona kwamba maumbile yenyewe yanaonyesha, katika jamii ya binadamu, dalili ya Kuja Kwake; kwa kuwa, wana wa Mungu, na binti za wanadamu wanakuwa warembo, na jinsi wanavyojitwalia wanawake. Ni saa ya jinsi gani tunayoishi! Loo, jamani, na jinsi ilivyokuwa katika siku ile!

⁹⁸ Halafu tunaona katika historia ya jambo hili kubwa la kutisha, la wanaume wakiwaabudu wanawake, na tunaona kwamba siku hizi ni ulimwengu wa wanawake.

⁹⁹ Nilikuwa Switzerland, si muda mrefu uliopita, na nilikuwa nikizungumza na... Sasa, sina neno dhidi ya wanawake wetu Wakristo, la, bwana, wao ni lulu. Ninazungumzia kuhusu mwenendo wa ulimwengu. Kulikuwa na bibi aliyekuwa anasafiri pamoja nami kwenye gari, Ndugu Guggenbuhl, na mpenzi wake ambaye alikuwa akisafiri naye. Yeye ni mtu wa kama—kama karibu umri wangu, hajaoa, mzee kapera, na alikuwa anatembea na bibi mdogo. Ndipo basi mmoja wa wasichana kutoka kule, naye alisema, “Ndugu Branham, twambie kuhusu Marekani. Tunasikia kwamba, wanawake kule, ni ulimwengu wa wanawake kule, bila shaka.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli.”

Kasema, “Sikuzote nimetamani kwenda.”

Kisha nikaanza kuwaelezea. Akasema, “Ati nini?” Nikasema, “Ndiyo.” Ilibadilisha wazo lake mara moja.

“Vema,” akasema, “ungewezaje kuishi maisha ya Kikristo mahali kama hapo, basi?” Fikiria hilo.

¹⁰⁰ Nilipokwenda kule—kule Rumi, na nilikuweco chini huko San Angelo, yale mapango ya kuzikia watu, lilikuwa linashtusha. Nilipotoka kwenye hoteli yangu na kushuka kwenda mahali panapoitwa, “Sarafu Tatu Ndani ya Chemchemi,” wanawake barabarani, jinsi walivyokuwa wachafu. Wanawake wanatoka na kukuomba uwape miadi, wa kila aina, kimo, sampuli. Basi nasahau ni wangapi waliomjia Billy na mimi na Ndugu Baxter, kabla hatujakifikia kile kidimbwi, pamoja na yule mtu wa TWA ambaye alikuwa anatuongoza. Nikasema, “Hivi inawapasa wanawake hawa kuishi namna hiyo?”

¹⁰¹ Akasema, “La, wakati askari walipokuwepo hapa, walilizoea jambo hilo. Na, hata hivyo, wana kazi nzuri, na bado wanaendelea.”

Lakini hata mahali kama hapo, nilipofika sehemu ya San Angelo, ule ubao mkubwa pale, kutoka Vatican, uliosema, “Tangazo kwa wanawake wa Marekani! Tafadhalini vaeni nguo kabla ya kuingia humu, mpate kuwaheshimu wafu.”

¹⁰² Nilimwona msichana wa Kimarekani aliposhukia Paris, ambapo ni, kwa kweli, moja ya mitindo yetu ilikuwa inatoka Paris. Bali msichana yule alikuwa amevalia kizinifu sana, akiwa na mama yake na baba yake, mpaka askari waliokuwa wanafanya kazi nje kule waliangusha sululu zao na vikoleo vyao, wakakimbia kule kuangalia kituko hicho, kumwangelia huyu msichana wa Kimarekani akipita.

¹⁰³ Sisi tunaongoza katika mitindo. Ambapo, ilikuwa Paris, bali sasa wanakuja humu kuokota takataka, uchafu mtupu. Na taifa hili, ambamo ndiyo kwanza ufufuo upite, wa ubatizo wa Roho Mtakatifu, huku mpenzi Bwana Yesu akionyesha ishara Zake na maaajabu ya rehema, na juu ya kunena kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, huku taa zikimulika huku na huko. Mungu ambaye anaweza kufufua mfu kutoka katika kitanda chake; Mungu awezaye kuwaponya wagonjwa; Mungu anayeweza kutabiri mambo kabla hayajatukia, na kuyafanya makamilifu kabisa, kila wakati, bila kushindwa. Nawe unaweza kuwahubiria wanawake wetu wa Marekani, nao wanazidi kuwa wabaya zaidi kila mwaka.

¹⁰⁴ Huko Bombay, namaanisha huko Durban, Afrika Kusini, ambako kulikuwa na wananchi mia mbili elfu wamekusanyika mkutanoni, wakati ulipotukia muujiza mkuu uliotendwa na

Mungu. Nami niliona wananchi thelathini elfu wanaovaa mablanketi. Wanawake wamesimama pale wamevikwa kitambaa kidogo cha inchi nne cha shanga tu ambacho kilining'inia humu mbele. Nao wanaume, hawana nguo, kitambaa kidogo cha shanga cha inchi nne. Uchi! Blanketi waliyolalia, ngozi ya mbuzi; wanapewa hiyo, wao, wanapofikia umri fulani; basi wanavaa hiyo, hulala nayo, hujifunika hiyo, wanapokufa huzikwa nayo, kwenye zizi la ng'ombe mahali fulani.

¹⁰⁵ Nami niliwaona hao wanawake, watu wa nyuma kwelikweli, hata mwanamke mmoja akazaa mtoto mchanga, huku ameketi futi ishirini toka nilipokuwa. Hakwenda kamwe hospitalini. Wao na mwanawake fulani walimsaidia hapo mara moja, na mnamo dakika tano yote yamekwisha. Akakichukua kile kitoto akakishikilia kifuaani mwake, kipate kunyonya. Ni wa nyuma namna hiyo! Bali walipoona uwezo wa Mwenyezi Mungu ukija juu ya mvulana ambaye alikuwa anateseka sana, na hata hakuwa na akili timamu; naye akainuka akiwa na akili timamu, akimsifu Mungu; wananchi thelathini elfu waliovaa mablanketi wakampokea Yesu Kristo kama Mwokozi. Kulitukia nini? Kumbukeni, hilo ni jambo kubwa kuliko Pentekoste mara kumi. Thelathini elfu! Na hakuna mtu...

Niliwaangalia wanawake wale kwa macho yangu, walipoanguka ardhini, huku wanavunja sanamu zao, wakiyatao maisha yao kwa Yesu Kristo. Hawakujua. Pengine hawajawahi kusikia Jina Lake, wengi wao. Bali walipiga ma—magoti yao, nami nikawauliza, kama walikuwa waaminifu kwa hilo, kama walilikusudia, wavunje sanamu zao. Basi wakavunja sanamu zao. Ndipo walipopiga magoti yao wakayatoa maisha yao kwa Kristo, nilipokuwa ninawaombea, wakainuka. Na hao wanawake ambao wangesimama huku wameshusha mikono yao chini, bila kujua walikuwa uchi; mara tu Uhai wa Kristo ulipoyagusa maisha yao, niliwaona wanawake hao wakikunja mikono yao na kuondoka mbele ya wanaume. Na kama mguso wa Yesu Kristo utafanya hivyo kwa mwananchi aliyevaa blanketi, yapasa ufanye nini kwa taifa ambalo limesikia Injili kwa mamia ya miaka? Hapo sisi sasa... Niliona jambo hilo. Hilo si jambo alilosema mtu mwingine. Niliona hilo. Unaona? Ni ajabu basi kwamba tunajiita wenyewe Wakristo, na kila mwaka tunavua nguo zaidi. Nayo makanisa yanaonekana hayajali kitu.

¹⁰⁶ Vipindi vya TV, loo, kuonyesha miili na damu ya wanawake... Wao si miungu. Wao si miungu ya kike. Bali linauweka Marekani sawa kabisa katika utaratibu ipate kutimiza Maandiko. Nambari ya Marekani ni kumi na tatu. Madhabahu ya Marekani ni mwanamke, sikuzote. Liko kwenye fedha zetu. Liko kwenye kila kitu. Na sasa hakika unakuja wakati ambapo tutakuwa na mungu wa kike wa Kimarekani,

pia, si mbali sana. Mnaweza kuyaona yale maandiko kwenye ukuta.

¹⁰⁷ Loo, tutafanya nini? Huwezi hata kutembea barabarani na kuona... Angalia barabarani, shuka uende katikati ya mji na utaona maonyesho wazi ya wanawake, jinsi ambavyo wanajishonea nguo za aina hiyo, kwa kweli jamani, mwanamke apaswa kuona aibu akisimama hivyo kwenye chumba chake cha kuvalia. Akitembea barabarani, zimembana sana, akiwa—akiwa amevaa nguo fupi sana. Na—na nje huku ufukoni wanakoogelea na hizi 'kini, sijui mnaziitaje, wamezivaa, na vitu kama hivyo. Huku hawajui kwamba ndani yao mna pepo mchafu. Ambapo, wengi wao huimba katika kwaya. Hicho ndicho Yesu alisema kingetukia.

¹⁰⁸ Miili ya wanawake! Wao ni mwili na damu. Wao si miungu. Kwa maoni yangu... Mungu anisamehe iwapo nimekosea. Ni kuvua nguo kabisa hadharani. Ni vigumu kumlaumu mwanamume, kama yeye si—si Mkristo, iwapo ataanguka, na kuanguka majaribuni na kufikia mahali ambapo angetenda kitu kibaya, hata ange... mnaona, hangeweza kujizuia. Ajabu ni kwamba hakuna unajisi mwingi zaidi unaotukia, kwa sababu, mara nyingi, wanawake ndio wana hatia. Bali, kama siyo ilivyo, ungewezaje kumlaumu mwanamume? Weka lawama mahali pake.

¹⁰⁹ Mwanamke anasema, "Sasa, Ndugu Branham, mimi ni mwadilifu tu kama ni..." Hapana shaka kuhusu jambo hilo.

Bali, dada yangu, unajua kwamba utawajibika Siku ya Hukumu kwa kufanya uzinzi unapojianika huko hadharani na wanaume wanakuangalia? Yeye alisema, "Ye yote atakayemwangalia mwanamke akamtamani, amekwisha zini naye moyoni mwake, naye atapasiwa hukumu kwa jambo hilo." Na pengine hukutenda kitendo kile, bali kama ukimruhusu Shetani kuweka roho yule juu yako, ambapo, maumbile yenyewe yapaswa kukufundisha ya kwamba hilo ni kosa! Bila Roho wa Mungu, maumbile yanapaswa kufanya hivyo, kukufundisha kwamba ni kosa.

¹¹⁰ Ninabashiri kwamba hivi karibuni watatoka na kimoja cha vitu hivi, itakuwa tu jani la mtini tena. Nilibashiri hilo miaka thelathini iliyopita. Unaona, wanaitusi Biblia. Unaona? Watafanya hivyo. Ni kuvua nguo hadharani.

¹¹¹ Sasa, ibilisi anafanya vile vile kwa wana wa Mungu leo. Na hiyo ni kweli. Angalia shughuli zetu. Karibu shughuli zetu zote zinatawaliwa na wanawake, shughuli nyingi. Hilo ni kweli. Angalia makanisa yetu, angalia taifa letu, jinsi wana wa Mungu wanavyosujudu kwenye madhabahu ya mambo haya, wanawake hawa. Ambapo, wao, kwangu mimi, wao si kitu ila makahaba wa hadharani. Hilo ni jambo baya sana kusema, bali ni kweli dhahiri. Najua kwamba watu husikia kanda hizi na kadhalika,

watasema mambo haya. Lakini waweza kufanya hivyo? Kama ukijionyesha namna hiyo, na mwanamume akuangalie, kama Yesu alivyosema wewe “umezini” naye. Na mwanamume huyo itakapompasa kujibu kwa ajili ya kufanya uzinzi, nani aliyefanya hivyo, ni kosa la nani? Ni huyo mwanamke aliyevua nguo zake namna hiyo na kujianika hadharani, au kujipeleka mbele ya huyo mwenye dhambi. Hiyo ni kweli. Ni ishara ya nini? Ya wakati wa mwisho, taa nyekundu.

¹¹² Umama umevunjika. Mataifa yanavunjika. Sasa iwapo unataka kuona ambapo Yesu alisema hivyo, soma Mathayo 5:28. Hapo ndipo ilipokuwa. Maisha ya wanawake ndiyo yamekuwa chanzo na hali ya kuanguka juu ya...hiyo nguvu ya kujuana kimwili ndiyo iliyosababisha uharibifu...Iwapo unataka kufuatilia, haya ni baadhi ya mataifa ambayo niliyafuatilia kule nyuma katika kuanguka kwao. Moja lilikuwa Misri, Ashuru, Rumi, na kadhalika, yaliangushwa na nguvu za wanawake.

¹¹³ Angalia, hakuna kitu ambacho Mungu angeweza kumpa mwanamume, nje ya wokovu, kilicho bora kuliko mke mzuri. Hakuna mwanamume anayeweza kufariji, hakuna—hakuna mtu anayeweza kumfariji mtu wanapokuwa wachovu, hawatamtegemea ye yote kama wanavyowategemea wake zao. Na ni bahati jinsi gani kwenu ninyi ndugu mnapokuwa na maskini mke mzuri ambaye ni msafi na mwaminifu, na mwadilifu, nawe unaweza kuja ukiwa mchovu na umedhoofika, ukaketi chini naye akakuzungumzia. Anaweza kukutendea mengi kuliko mtu ye yote yule. Hilo ni kweli. Yeye ni lulu. Ni malkia.

¹¹⁴ Bali kumbuka, “Mwanamke alifanywa kwa ajili ya mwanamume; si mwanamume kwa ajili ya mwanamke.” Kiumbe cha mwisho cha kuumbwa ambacho Mungu aliumba kilikuwa mwanamume. Mwanamke ni kitu kilichotokana na mwanamume. “Naye aliumbwa kwa ajili ya mwanamume; si mwanamume kuumbwa kwa ajili ya mwanamke.” Wameligeuza jambo hilo, nao wanaume wanasujudu kwenye madhabahu ya wanawake. Hicho ndicho kitu kile hasa kilichosababisha jambo hilo hapo mwanzo. Hicho ndicho kilichotukia hapo mwanzo. Ambapo mwana wa Mungu, Adamu, hangeweza kujaribiwa kufanya kosa. Shetani aliingia ndani ya mtu aliyeitwa nyoka, ambaye alikuwa kama mwanadamu. Na hapo ndipo lilipoanza, ambapo Hawa alitoka nyuma ya Neno la Mungu, ndipo jambo hilo likasababisha kila huzuni, kila kaburi. Kila dhambi iliyowahi kufanywa, ilianza papo hapo.

¹¹⁵ Hili hapa tena. Nini? Wanawake ndio waliosababisha kule kuanguka kwa kwanza, pia wanawake ndio watakaomaliza wakati. Mwanamke ndiye aliyeanzisha; ndiye anamalizia. Si ajabu Biblia ilisema, “Nao watakaookoka katika Sayuni watatukuka mbele za uso wa Bwana.”

¹¹⁶ Wakati Isaya 5, alipozungumzia ambavyo tabia mbaya za wanawake zitakavyokuwa katika siku za mwisho, na jinsi kungekuwa, wangukuwa na nguo kiasi gani, na jinsi ingewalazimu kutengeneza nywele zao, na kila kitu namna hiyo. Biblia huzungumzia jambo hilo, Isaya 5. “Jinsi angetembea na viatu vyenye visigino virefu, anakwenda akiliza njuga kwa miguu yake. Na angeteremsha soksi zake ndefu, na mambo ambayo angetenda; na jozi nyingi za kubadili, nguo, na viatu kama hivyo.” Kisha kasema, “Yote hayo yataondolewa kwake, naye ataketi na kutoa uvundo, kwa ajili ya ufisadi.” Tena kasema, hata, “Wanawake saba watamshika mtu mume mmoja, waseme, ‘Tutafanya kazi yetu. Lakini na tuitwe tu kwa jina lako; utuondolee aibu yetu.’”

¹¹⁷ Bali alisema, “Jinsi litakavyokuwa lenye utukufu chipukizi lile ndogo litakalookoka na yote haya! Litakuwa ‘UTAKATIFU KWA BWANA’ katika siku ile,” wakati wanawake waliozaliwa kweli mara ya pili watajua mahali pao, ingawa watachekwa, na kuitwa wajinga na wa mtindo wa kikale na kila kitu. Bali, enenda kama mwanamke, kama bibi! Simama kama mwanamke! Vaa kama mwanamke! Zungumza kama mwanamke! Ishi kama bibi, katikati ya mambo hayo kabisa. Ndiyo. Amina. Hilo, humaanisha tu, “na iwe hivyo.” Usifadhaike. Haikumizi. Sawa.

¹¹⁸ Neno la Yesu Mwenyewe lilisema ambalo lingetukia, onyesho hilo kuu.

¹¹⁹ Pia Yeye alisema, “Katika siku za Lutu.” Kama ukitaka kutia alama Andiko hilo, ni—ni Luka 17:28. Yeye alisema, “Walikuwa wakila, kunywa. Walinunua. Waliuza.” Kwa kawaida, haya ni mambo halali. Bali angalia. Basi wao walifanya hayo, lakini waliweka yote. . . akili yao kwenye hilo.

¹²⁰ Na katika siku za Lutu, wanawake walikuwa duni sana, katika maadili yao, hata hawakutumiwa jinsi wanawake wanapaswa kutumiwa, bali walikuwa wamepotoshwa, mpaka wao. . . Lilikuwa jambo la kawaida sana, kwamba wanawake walikuwa kitu cha kawaida sana hata, wao—wao, wanaume walilala na wanaume wenzao. Huo upotovu wa kiasili uliziondoa chembechembe za kujuana kimwili mahali pake, kwa sababu wanawake wamekuwa rahisi sana.

¹²¹ Siku chache zilizopita nilikuwa huko, Tucson, nikaenda kununua mkate. Basi palikuwa na mvulana ameketi nje kule, na wavulana wadogo wawili kwenye gari ndogo. Mwingine akaingia kununua pakiti ya sigara. Mzee mwuungwana aliyekuwa na mvi akatazama chini, akasema, “Hizi sigara ni za nani, mama yako?”

Kasema, “La, ni za mvulana yule.”

Kasema, “Ni mkubwa vya kutosha kuzitumia?”

Kasema, “Ndiyo, Bwana.”

Akatazama nyuma namna *hiyo*. Nami nilikuwa nimesimama na na kisaga kimoja cha maziwa, nikiangalia. Naye akaondoka, akasema, “Sawa,” naye akampa hizo.

Akageuka kunitazama, kasema, “Ninatilia shaka hilo.”

¹²² Nikasema, “Hawezi kuwa mkubwa vya kutosha kuzitumia. Ni mdogo sana . . . Hana umri wa kutosha katika umri wo wote.”

Akasema, “Nitakubaliana nawe.” Kasema, “Unaona—unaona shida kujaribu kuachana nazo?”

¹²³ Nikasema, “Sijazianza kamwe.” Nikasema, “Sijazianza kamwe.” Nikasema, “Wazazi wangu walivuta sigara na kutumia tumbaku, bali Bwana Mungu ameniepusha nazo.”

¹²⁴ Akageuka na kuniangalia kwa mshangao, akasema, “Naam, nafikiri ni aibu sana leo, kuona jinsi . . .” Kasema, “Hapo zamani, tuliwaheshimu sana wanawake.” Kasema, “Tulimheshimu mwanamke. Tulivua kofia zetu mbele zake. Tulitembea barabarani, na kama muungwana angemsikia mtu akimkashifu mwanamke, wangalimpiga kofi wakamwangusha chini.” Unaona? Akasema, “Waliwaheshimu wanawake.” Lakini akasema, “Bwana, wanawake wamejidhulumu wenyewe.” Kasema, “Sasa hawainuki. Walikuwa na desturi ya kusimama; kwenye mabasi, bibi akisimama, kila mwanamume angetoa kofia yake na kumwachia kiti.” Kasema, “Sasa ni kusukumana, kusongamana!” Kasema, “Wamejidhulumu wenyewe.” Na hiyo ni kweli.

Lile tundu la ibilisi la huko Hollywood liliyabuni kwenye televisheni na magazeti, mpaka jambo hilo limekuwa chungu kubwa mno la uchafu. Hiyo ni kweli.

¹²⁵ Najua huo si usemi unaopendwa sana na watu, lakini ni maneno ya kweli. Ni Kweli. Ni Neno la Bwana, na pia ishara ya kuonya kwamba Kristo atakuja katika kizazi hiki. Kasema, “Wale watakaona haya yakitimia, hawatapita mpaka mambo yote haya yatimizwe.” Kasema, “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe.” Ni onyo. Taa nyekundu inamemetesha; inatelemsha pazia. Tuko katika wakati wa mwisho.

¹²⁶ Tunaona ishara za Bwana Yesu akiponya wagonjwa, akifufua wafu, akitoa pepo wachafu. Tunaona wa—watu wakifanywa watauwa na watakatifu, na Roho Mtakatifu. Tunaona maisha yakibadilishwa. Tunaona ishara kuu. Tunaona ishara za ajabu angani, kama visahani vinavyoruka. Pentagon, watu wengi wakiliweka kwenye televisheni, wakiandika habari zake. Hawajui wafikirie nini kuhusu jambo hilo. Aina zote za ishara za ajabu! Bwana Yesu akishuka katika Nguzo ya Moto, Naye akipigwa picha, akiishi miongoni mwetu, akithibitisha kwamba ni yeye yule jan . . .

¹²⁷ Tunaona mambo yote haya yakitukia. Tunaona ubaridi wa kanisa. Tunaona madhehebu yakistawi. “Muonapo mtini, na ile miti mingine yote ikichipua matawi,” Wayahudi wakirudi. “Mtini.” Wayahudi wakirudi kwenye taifa lao, nchi yao wenyewe. Tunawaona Wapresbiteri, Wamethodisti, Wabatisti, Waluteri, Wapentekoste, makanisa yote, “Yakichipusha majani,” *ufufuo*. Akasema, “Jitayarisheni! Huo ndio wakati.” Tunapoonaa hilo likitimia, hapo ndipo Mungu anajitayarisha kuita Wateule Wake. Basi wakati ninyi. . .

Ishara nyingine. Kasema, “Mtakapoonaa wanawake wakiwa warembo sana, mtakapoonaa wana wa Mungu wakijitwalia wanawake, na kujitwalia wanawake, na kufanya *hili, lile, au jingine*,” kasema, “jueni kwamba hiyo ndiyo ishara.” Tumefika.

¹²⁸ Sasa, kitu kingine nilichokuwa nimeandika. Kumbuka wale binti wawili wa Lutu. Ndiyo, tunawakumbuka, huko kwenye jiji la Sodoma. Yesu alisema hapa, katika Luka 17, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma.” Kumbuka, kwamba, wanaume walikuwa wamewatumia wanawake kwa jinsi isiyo ya asili ya maisha hata tendo hilo halikutamaniwa tena. Na, loo, ni vibaya sana kunena hili jukwaani, lakini hii ni. . . Kukiwa na Kweli yo yote, yapaswa itoke hapa. Na ni mbaya mno, leo, mpaka kuna makumi elfu mara elfu yao, wanaongezeka kila mahali, upotovu, Walawiti, kama ilivyokuwa katika siku ile. Kwa sababu matumizi ya asili ya maisha ya binadamu kuzaana duniani yamedhulumiwa sana, na yameharibiwa sana jinsi mambo yamekwenda, hata tamaa ya tendo hilo imepungua haraka sana. Nitasema, mnamo miaka mingine kumi au kumi na mitano litakuwa karibu limepita, jinsi jambo hilo linavyoongezeka sasa.

¹²⁹ Matamshi makubwa. Nilikuwa na kitu fulani toka kwa Edgar Hoover kuhusu hilo, bali sijui. . . Nilifikiri nilikuwa nacho hapo, bali sina, juu ya yale aliyosema kuhusu jambo hilo. Na sasa tunaona mambo haya. Loo, jamani!

¹³⁰ Yuda, katika Kitabu chake kidogo, kikubwa, ninakiita hivyo, katika aya ya 7, hebu tuisome. Nataka kuisoma. Yuda, katika aya ya 7. Hiki ni Kitabu cha mwisho kabla ya Kitabu cha Funuo. Nimeitia alama hapa, Yuda 7, aya ya 7. Mwanamume na mwanamke wakitoa nadhiri za ndoa, wakizivunja, wakienda kufuata mambo ya mwili yasiyo ya asili! Sikilizeni.

. . . *kama vile Sodoma na Gomora, na miji iliyokuwa kando-kando, waliofuata uasherati kwa jinsi moja na hawa. . . kaenda kufuata mambo ya mwili yasiyo ya asili. . . (Unaona? Loo.) uasherati. . . wakaenda kufuata mambo ya mwili yasiyo ya asili, imewekwa kuwa mfano, wao wakiadhibiwa, na moto wa milele. (Yaani, kuteketewa kabisa na kuangamizwa.)*

¹³¹ Hapa wakati mdogo uliopita, huko Los Angeles, nilikuwa nikingojea, au nilikuwa kwenye kambi. Nilikuwa ninaendesha

barabarani. Na ki—kijana mwanamke, msichana mdogo mzuri, mrembo sana, alikuwa akitembea barabarani. Nami nikawaza, “Yeye lazima anaenda kuona sinema.” Naye alikuwa amevaa nguo za kimagharibi, upana wa kama tu—kama inchi sita au nane kufunika upande wake wa mbele, na matamvua yanayoning’inia inchi tatu au nne. Na juu kabisa mwilini mwake, kipande fulani kidogo, karibu tu ungeliweza kukishindilia chote katika konde lakoni, kikining’inia kumzunguka namna *hii*. Akivalia kofia ya cowboy, na buti zenye vishada. Na ni wa kuvutia sana, ningeweza kuona ambapo kijana mwanamume ye yote angefunga breki na kila kitu, kusimama alipo, akienda kwa hatua za madaha barabarani.

¹³² Nami nilikuwa ninajiandaa kuelekea kwenye kambi, basi nilipanda nikaelekea kambini. Ndipo nikaanza kugeuka, kurudi. Nikafikiri ningesimama, niseme, “Kijana mwanamke, nataka kuzungumza nawe katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Ingawa u msichana mrembo, hapana shaka kuhusu jambo hilo, ingawa una umbo ambalo labda . . . Wewe, unataka kusikia breki zikilia. Unatambua ya kwamba pepo anayekufanya wewe ufanye hivyo atakupeleka jehanum kwa ibilisi ambako utateswa katika nyakati zijazo? Unatambua kwamba huo mwili mzuri na mdogo ulioubika vilivyo, na hayo mashavu yaliyokaa vizuri pamoja na hizo nywele, na kadhalika, na midomo myekundu, pengine katika—katika miezi sita ijayo mabuu yatatambaa ndani na nje ya huo mwili ulioubika vizuri, na nje hapa mavumbini? Na nafsi ile ambayo inakaa humo, leo, itakuwa kwenye mateso ya ibilisi.”

¹³³ Kisha kitu fulani kikanikataza, kama kwamba Mungu angesema, “Kama ukifanya hivyo, watakufunga ndani kule gereza.” Unaona? Basi. Kisha nikamwona Billy akitoka na kunipungia mkono, wakati wa kuja umewadia. Nikawasikia wakiimba *Amini Tu*.

¹³⁴ Loo, jamani! Watu wanawezaje kurogwa na upuzi kama huo? Ni kwa sababu wanalipuza Neno la Mungu.

¹³⁵ Na jambo jingine, ni wahudumu nyuma ya jukwaa, ambao wanashiriki katika madhehebu haya, ambao wanasoma Hilo na kujua jambo Hilo, nao wamekatazwa kusema jambo lote kuhusu Hilo, kwa sababu watalifanya kusanyiko lao liwaache basi. Na makanisa yanatafuta washiriki. Bali Mungu anawatafuta watakatifu wa Mungu waliozaliwa mara ya pili, ambao watang’aa kama nyota. Mungu na atusaidie kuwa waaminifu na kusema Kweli, yale aliyosema Yesu Kristo. Lakini hiyo ndiyo siku ambayo tunaishi. Hizo ndizo ishara ambazo Yesu alisema zingekuwa, na tunaona jambo hilo papa hapa mbele yetu.

¹³⁶ Angalia sasa, Yuda sura ya 7 tena, “Sodoma na Gomora.” Loo, jamani, jambo la kutisha jinsi gani! Wasiooa wanawake,

“wakienda kufuata mambo ya mwili yasiyo ya asili.” Mwanamume aliyeoa mkewe, wao ni—wao sio wawili tena, ni mmoja. Na mwanamume atakayemfuatilia mwanamke mwingine, yeye basi papo hapo anajitenga na mkewe. Na mwanamke ambaye atatembea na mwanamume mwingine, amekufa kwa mumewe. Ameukana mwili wake mwenyewe, amekatiliwa mbali naye. Hilo ni kweli. Siku ya Hukumu, atapatilizwa hukumu, kwa tendo hilo.

¹³⁷ Lakini leo hawataki kusikia Ujumbe kama huo. Watu hawataki kuusikia Huo. Wanataka kutekenywa katika maskio yao. Sawa kabisa na yale Roho Mtakatifu aliyoniambia siku ile nilipoliweka lile jiwe la pembeni pale, kasema kwamba:

Lihubiri neno; uwe tayari, wakati ukufaa na wakati usiokufaa, . . .

Maana utakufa wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe wata . . . watakusanya pamoja waalimu makundi-makundi, kwa kuwa wana maskio ya utafiti;

. . .nao watajipusha kutoka kwa ile kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo.

Kasema, “Ono litakapoondoka, soma Timotheo wa Pili 4.” Kasema, “Usisahau, Timotheo wa Pili 4!” Na ono lile liliponiacha, nikiwa nimesimama katikati pale kwenye Barabara ya 7, mvulana wa miaka kumi na tisa akisimama pale, Sauti ya Mungu ilinena chumbani, Naye akasema, “Timotheo wa Pili 4.” Hivyo ndivyo imetukia hasa. Unaona? “Utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima.”

¹³⁸ Watu wanataka jambo fulani. Wapentekoste wanataka kitu ambacho kinaweza kuwabembeleza, na kuwaacha waishi jinsi wanavyotaka kuishi. Nao wanaweza kucheza piano mapigo arobaini kwa sekunde, kurukaruka juu chini, na kucheza—cheza; na wanawake watende wanavyotaka, na wanaume vile vile. Mpresbiteri, Mmethodisti, Mluteri, na Mbatisti, wapo watu wengi waaminifu katika madhehebu hayo yote. Hilo ni kweli kabisa. Bali utaratibu ule umewafunga sana, mpaka wanafikiria maadamu wao ni washiriki wa kanisa lile, na majina yao yamo kwenye vitabu vile, kwamba wanaelekea Mbinguni. Kuweko kwa jina lako kwenye kitabu hapa duniani, halimaanishi *hilo* Kwake Mungu. [Ndugu Branham alidata kidole chake—Mh.] Jina lako lapaswa liandikwe kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, kwa Damu ya Yesu Kristo, kujua kwamba dhambi zako zimesamehewa. Hiyo ni kweli.

¹³⁹ Bali wanataka aina hiyo. Wao wanataka kuwaleta wachungaji kama hao. Hawataki kitu kingine. Na wakati Mungu katika siku hizi za mwisho amekung’uta kila kipawa cha Mungu ambacho kimesifiwa katika Biblia, kila kipawa ambacho Yesu Kristo aliahidi, kila kipawa, na kila ishara, kila ishara ya wakati

wa mwisho. Kila kitu ambacho kiliahidiwa katika Biblia, kadiri ninavyoweza kuona, mimi mwenyewe, kimekung'utwa mbele ya taifa hili, nalo linaendelea kutumbukia kuelekea jehanim upesi liwezavyo kwenda. Eti uwaambie? Wataendelea, kwa vyo vyote.

Hebu nichukue Maandiko mengine machache hapa kabla sijafunga. Vema. Loo, "Wamewekwa wapate kuangamizwa Milele," ndivyo walivyo, Biblia inasema.

¹⁴⁰ Taifa hili linakaa katika uvundo uu huu. Uvundo uu huu wa watu, taifa hili linakaa mle usiku wa leo. Mnajua hilo. Si mzaha. Si uzushi. Ni Kweli. Mwanzo 6:12, "Kila mwenye mwili ameharibika, binadamu amepata njia yake," katika mawazo yake mwenyewe, akipuza amri za Mungu. Hivyo ndivyo binadamu wanavyotenda leo. Mwanadamu hataki kusikia Neno la Mungu. Watu hawataki kusikia Hilo. Wanataka wapitie njia yao wenyewe.

¹⁴¹ Yezebeli alikataa kusikiliza Neno la Bwana. Asingetaka kumwita yule mhubiri mzee wa kale aliyejaa malaika, Eliya, mchungaji wake. Lakini alikuwa mchungaji wake, hata hivyo. Sawa. Mungu alimtuma, naye akauvumisha ujumbe wake. Ingawa hakupata elimu, hawajui alikotoka na alikokwenda. Alijitokeza uwanjani na Neno la Bwana. Alituma ujumbe wake, ambao aliuhubiri, na akahukumu kila kitu kilichokuwepo, kiitwacho dhambi. Huyu, huyo Yezebeli wa kisasa, amewaburuga na kuwaloga watu kwa uchawi wa nguvu zake mpaka taifa lote likaharibika, naye Eliya alisimama peke yake nje huko kwenye mlima. Mungu akasema, "Eliya, usiwazie jambo hilo. Ninao elfu saba chini kule ambao ni waaminifu moyoni, bado." Huo ni mvuto wake wa pili, na ule wa tatu ulienda kuwatafuta.

¹⁴² Lakini kumbuka, Mungu alikuwa amejaa rehema, na Yeye—Yeye... Na Ujumbe wa Eliya ulikihukumu kile kizazi kisichoamini. Ujumbe wa Nuhu ulikihukumu kizazi kile, na ukaleta hukumu juu ya wale waliokataa kuusikia, na ukombozi kwa wale waliouamini. "Na kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, hivyo ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu."

¹⁴³ Mwanzo 6, kutojali amri za Mungu! Wao husema, "Amri za Mungu?" Neno la Mungu linasema leo, katika Biblia!

Sasa sikiliza, sineni hili kwa mtu ye yote binafsi. Ninawajibika tu, kama ndugu yenu, ninawajibika kwa kuwaambieni Kweli yote, kama yule mtakatifu maarufu Paulo alivyosema kabla ya kuondoka kwake, "Sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu."

¹⁴⁴ Sasa, Biblia husema, leo, kwamba wanawake hawapaswi kukata nywele zao. Sijali ni wahubiri wangapi wanasema kwamba hilo ni sawa; ni kosa. Sijali ni makanisa mangapi

wanaliunga hilo mkono; Biblia ingali inasema kwamba hilo ni kosa. “Ni aibu kwake kufanya hivyo.” Lakini wanaendelea kulitenda hilo, haidhuru, wanaendelea. Wanafanya nini? Katika akili yao wenyewe, wakijirembesha wenyewe, wanadhani ni warembo.

¹⁴⁵ Neno la Mungu linaonya, asitende mambo haya. “Asivae nguo, au suruali, au cho chote kinachompasa mwanamume,” bali hata hivyo anaendelea tu. Jaribu kumkataza?

“Kwa hiyo, mbona unapiga makelele basi, Ndugu Branham? Mbona unaendelea? Mbona, watu watakupenda vizuri zaidi iwapo. . .” Mimi sijali, jambo hilo. Ninajali wanalofikiria watu. Sasa msinieleme vibaya. Bali ninapendelea ambalo Mungu anafikiria, na *hili* ni Neno Lake.

Ndiyo, unamwambia ni kosa kufanya hivyo, ataendelea moja kwa moja na kulitenda, haidhuru. Unaona? Kwa nini? Wanawake katika jamii yote ya Wakristo hutenda mambo haya, na kanisa halionekani kujali kamwe. Mbona hivyo? Wana wa Mungu wameanguka kwa tamaa mbaya ya mwili na damu ya wanawake, na kumkana Mungu yeye yule na Damu ambayo imewanunua, ikawatenganisha wao na mambo hayo machafu. Amina. Hiyo ni Kweli. Kwa hiyo Mungu nisaidie, ni Kweli.

¹⁴⁶ Jaribu kumkataza? Unadhani mahubiri ya Nuhu yaliwazuia kamwe? La, bwana. Lakini ni nini? Ni sauti, Sauti ile. Na wakati sote tutakapoitwa kwenye Hukumu, Ujumbe uu huu ambao ninahubiri, usiku wa leo, utakutana nami kuko huko, Neno kwa Neno. Basi utafanya nini? Ni kimulimuli chekundu.

¹⁴⁷ Kulikuwa na wakati, ukaidi uliingia miongoni mwa wanawake. Tuta. . . Tutaweka hili, kwa sababu hii ni kwa wanawake. Na unashangaa kwa nini sikuzote nimekemea jambo hili. Sasa ninaenda, kuchukua mengi—Maandiko mengi yaliyowekwa kabla sijamalizia, na kuwaonyesheni kwa nini. Na hiyo ndiyo sababu yanibidi nidumu mwaminifu kwa Neno hili, na kila mtumishi wa Mungu yampasa adumu mwaminifu kwa Neno. Yakubidi udumu, kwa sababu yabidi kuwepo na sauti mahali fulani inayolia dhidi ya jambo hilo. Sijali wengine wanatenda nini; huwajibiki kwa ajili yao. Unajibu kama mtu binafsi. Hujibu kama Mmethodisti, hujibu kama Mbatisti, au Mpentekoste. Unajibu kama mtu binafsi, kwa Mungu, kwa ajili ya maisha yako.

¹⁴⁸ Basi tunaona ishara hizi, na bado wao wanaendelea kulitenda. Mwambie ni kosa, utaona atakachosema. Wakaidi! Hivyo ndivyo Hawa alivyofanya hasa. Hawa alijua haimpasi kutenda jambo hilo. Alijua? Alikuwa na Neno la Mungu. Kasema, “Siku utakayokula, siku hiyo utakufa.” Naam, kwa nini alilitenda? Alitaka njia yake mwenyewe. Na kwa nini wanawake wakate nywele zao; kwa nini wanawake wavae nguo hizi, na Biblia imesema kwamba hilo ndilo hasa wanalopaswa kutenda?

Na jambo wanalotenda, wote wamehukumiwa. Sawa kabisa. Lakini kwa nini analitenda? Ana mambo yake mwenyewe. Ndiyo, bwana. Atatenda anavyotaka mwenyewe. Na kanisa halisemi neno lo lote kuhusu hilo. Na kanisa lapaswa kuwa Bibi-arusi wa Yesu Kristo, basi lisiseme neno dhidi yake?

¹⁴⁹ Ukimwambia mmoja wao kuhusu jambo hilo, unajua wanasema nini? Kiasi cha kama kusema, “Hakuna Biblia ya kale itakayonizuia kujifurahisha.” Sasa ni sawa kabisa. Unawaambia imeandikwa kwenye Biblia. Loo, wanaweza wasiseme maneno hayo, bali hivyo ndivyo wanavyoonyesha.

Uliwahi kusikia ule msemu wa kale, “Matendo hunena kwa sauti kubwa kuliko maneno”? Vema, basi, yanafanya hivyo? Matendo hunena kwa sauti kubwa kuliko maneno. Haidhuru unasema nini, maisha yako—maisha yako yananena kwa sauti kubwa sana hata hao hawawezi kusikia ushuhuda wako. Kama nilivyosema asubuhi ya leo, ruka juu tu kadiri unavyoishi. Unaona? Matendo yako hunena kwa sauti kubwa kuliko maneno yako. Na afadhali hata utoke ukayanene, kwa sababu matendo yao wenyewe hunena. Maneno—maneno yako, haidhuru ni nini, matendo yako hunena u—ulivyo wewe.

Kama ukizungumza neno lo lote tofauti na ulivyo wewe hasa, inakuwa unafiki. Yesu alisema, “Enyi wanafiki! Mwawezaje kunena mambo mema, ambapo toka moyoni hunena, kinywa hunena yanayotoka moyoni?” Unaona, walikuwa wakisema kitu fulani wasichokimaanisha.

Na wanawake hivyo, ndio husema hivyo, loo, jamani, “Kujifurahisha mimi mwenyewe.”

¹⁵⁰ Kunatukia nini? Kutoka kwenye ndoa... Hapa ni mahali pengine katika Biblia. Kutoka kwenye ndoa hutoka nadhiri, “tii.” Kutii? “Mke wa nyumbani, mtakatifu, mwenye matendo mema.”

Anakuchekelea usoni na kwenda kwenye mtambo wa vipodozi, afisi ya mtu fulani. “Mume wangu...” Ndiyo. Loo, nalionea shaka jambo hilo.

Unaona majeshi leo, aibu jinsi gani, kuweka wanawake kwenye jeshi la polisi. Kama hiyo si alama ya—ya zinaa katika mji wo wote! Huku wanume wengi hawana kazi, na inawabidi kuwaweka hao wanawake nje huko, ambapo Biblia ilisema anapaswa “akae nyumbani na awe mtunza nyumba msafi.” Bali anatunza vitabu vyote vya bosi, na vyako pia. Ndivyo. Hiyo ni kweli.

Sizungumzi kuhusu wanawake walio wema sasa. Siwasemi ninyi wanawake ambao mu wacha Mungu. Mungu awabariki. Hilo liko kwenye kanda, au po pote pale.

Bali ninazungumzia kuhusu, ambapo unamkuta mmoja kama huyo, unawakuta elfu moja na mia tano upande mwingine.

Hawatalisikiliza Neno. “Kaa na Biblia yako! Jihubirie Hiyo mwenyewe. Hatutaki kuisikia.” Kutii? Loo!

¹⁵¹ Angeweza kusema hivi, “Zisimulie hadithi zako za Biblia mtu mwingine. Mweke Mungu wako kwa mtu mwingine, achana nami. Unanipigia mimi kelele za nini? Sijakuomba kamwe kusema mambo haya.” Najua, bali Mungu aliniagiza. Unaona? Kwa hiyo ni hayo tu.

¹⁵² Kwa hiyo bado wanaiharibu ile njia. Kama walivyofanya katika siku za Bwana, kama tu walivyofanya katika siku ile, ndivyo wanavyofanya leo, ni vile vile tu. Haijabadilika. Haibadiliki. Haitabadilika.

¹⁵³ Hatia za watoto hatimaye zinawapata watoto wake. Gereza linapata sehemu ya wanawake na wanaume, kisha kuzimu inakichukua kitu hicho chote, hilo ni sawa kabisa, hatimaye inawameza wote. Na mahubiri yanaonekana kama yanapitia juu ya migongo yao. Kamwe hawayasikilizi. Watafanya wapendavyo. Waweza uwaambie Biblia inasema *Hivi*. Waseme, “Kaa na Biblia yako. Tutajifurahisha wenyewe.”

¹⁵⁴ Naweza kuwasikia baadhi yenu dada mkisema sasa, pengine si ninyi mlio hapa, lakini nawasikia mkisema, “Nani, eti mimi nimtii mume wangu? Loo! Mimi humfanya yeye anitii.” Lakini hapo ndipo umekosea. “Eti nikae nyumbani msafi? Sijali Biblia inasemaje juu yake, usinisumbue!” Sikiliza, dada, hiyo haikuwa katika, kule nyuma katika zile Siku za Giza, hiyo ni sauti ya leo. Hilo kamwe halikutukia kule nyuma sana kabla ya ile gharika, linatukia leo pia. Hilo ni jambo lile lile.

¹⁵⁵ Tena wanasema, “Mimi ni mwanamke wa kisasa. Naishi Marekani.” Vema, hilo si bora kuliko kusema unaishi katika zizi la nguruwe. Mungu hangejali unakoishi wewe. Uko jinsi ulivyo moyoni mwako. Hiyo ni kweli. Na usifikiri, dada, eti wewe u wa kisasa sana, kwamba u mmoja wa hawa wanawake wa kisasa, kama mnavyotaka kusema leo. Umetoka huko nyuma kabisa, kulingana na Biblia hii, kwenye zile nyakati za giza, kabla ya ile gharika. Katika wakati wa Nuhu, hapo ndipo walipotenda jambo lile lile. Kwa hiyo wewe si wa kisasa sana, hata hivyo, sivyo? Unaona? Hivyo ndivyo walivyotenda katika ulimwengu uliotangulia ile gharika. Unaona? Na hivyo ndivyo wanavyotenda leo, kwa hiyo lazima iwe ni wakati wa giza tena, huko nyuma kwenye giza kuu.

¹⁵⁶ Nawe mwanamume ambaye utamwachilia mkeo afanye hivyo, ninyi si watoto wa Mungu tena. La, kwa namna fulani mlianguka katika Sodoma, hiyo ni kweli, mkawaachilia hao wanawake wawatawale kila mahali. Loo, jamani!

Sijui kama nilisema jambo hili au la. Afadhali niiache sehemu hii. Bali. . . Sawa. Hili ni baya sana.

¹⁵⁷ Lakini yote haya ni kwa wakati huu...?...Mnaona kimulimuli chekundu kikiwaka, kikimemetesha? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

Baragumu Yake Bwana wakati ikipigwa,
Na siku ya Milele ikifika;
Hapo waliokombolewa watakusanyika (toka
kwenye mavumbi ya ardhi),
(Loo, itakuwa siku nzuri jinsi gani! Sawa. Loo,
ndiyo!)

¹⁵⁸ Kurudi Sodoma? Usifadhaike, kuna makombora ya atomiki yanayongojea kuusafisha wote, hiyo ni kweli, kuusafisha ulimwengu mzima. Yataufanya hivyo. Na kisha wote utafanywa upya tena, kama tulivyoona chini ya Muhuri ya Sita, kwa ajili ya kundi la watu waliokombolewa ambao wamemkubali Bwana Yesu, ambao wamekuwa Wakristo, ambao wameuza shughuli zao zote na mitindo yao yote ya dunia hii, wakamjia Yesu Kristo, wanaomtumainia Yeye na Yeye pekee; kwenye utaratibu Wake mnyenyekevu na rahisi, wakaja wakamwamini Yeye, na kuupokea Uzima wa Milele. Na kama ukisema una Uzima wa Milele, na hukubaliani na Biblia hii, uzima wako wa milele si Uzima wa Milele unaotolewa na Mungu. Umedanganywa, na mauti, sio Uzima. Hiyo ni kweli.

¹⁵⁹ Sasa, loo, “Mche Mungu nawe ulishike Neno Lake, kwa maana hii ndiyo amri iliyo kamilifu.” Taa nyekundu zinamemetesha, na muda umekaribia. Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, unaona, walichukua kitu kilicho halali nao wakakipotosha. Walichukua kula, wakachukua kunywa, na wakashika kujenga, na wakayaweka mambo haya yote mengine, wakayapotosha. Sasa, Yesu anatutazamia kujenga makazi, unaona; bali angalia jambo ambalo limetukia katika tendo hilo. Kula, Yeye anatutazamia tule, bali angalia jambo ambalo limetukia katika tendo hilo. Kunywa, tunatazamia kunywa maji yetu na lo lote litupasalo kutenda; bali, badala ya tendo hilo, wameingilia kunywa pombe na vileo, na kila kitu, na vinywaji vikali, wakija na wanawake wao. Mnaona?

¹⁶⁰ Na vipi kuhusu ongezeko la watu, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu? Vipi kuhusu urembo wa wanawake kuongezeka bila kikomo, zaidi na zaidi? Unaona? Taa nyekundu!

Vipi kuhusu wakati ambao wanawake wangekuja, wakati ambao wangekuwa jinsi walivyokuwa, “wakaidi, wenye kujivuna,” na kila kitu, hungeweza kuwaambia kitu? Ukiwahubiria wao Neno, wataendelea tu kutenda hayo kwa vyo vyote. Unaona?

Itakuwaje? Sawa kabisa tu na ilivyokuwa katika siku za Nuhu. Siku moja, mlango wa rehema utafungwa. Ndipo Maandiko yanasema, “madhabahu yakafuka moshi,” maana yake ni kwamba Mwombezi ameondoka humo. Na maadamu

Mwana-Kondoo bado yuko nyuma kule... Kama nilivyosema asubuhi hii, au mahali fulani nilipokuwa ninahubiri, kwamba, maadamu Mwana-Kondoo yungali mle akituombea, bado kuna rehema. Bali ni matumaini gani tuliyo nayo, tuonapo gari moshi tayari liko jengoni, tunapoona Kuja kwa Bwana, ile taa ikimemetesha?

¹⁶¹ Jinsi ningeweza kuzungumzia kuhusu mambo mbalimbali tunayojua Yeye aliahidi kutenda hapa katika siku za mwisho, nasi tunalionga papo hapo mbele yao. Na halafu tunaona somo hili usiku wa leo, la kimulimuli kingine chekundu kikimemetesha, cha kufanya yasiyofaa miongoni mwa wanawake wetu, na jinsi wanavyotenda mambo. Tunaona ikionyesha, kila—kila hatua, kila kitu, kila sindano, kila dira, imeelekezwa kabisa kwenye Kuja Kwake. Tuko mwisho. Hakuna kitu kingine ambacho ninajua kitatukia isipokuwa Kuja kwa Bwana.

¹⁶² Ndipo basi, rafiki yangu mpenzi uliye nje ya Kristo, unaliwaziaje jambo hili? Unakaa tu... Kwa kweli, rafiki, nataka kukuuliza swali rahisi. Unakaa ukitumainia msisimko fulani ulioupata, au baadhi, pengine, kitu fulani ulichowahi kuwa nacho? Pengine uliona furaha wakati mmoja na ukacheza kila mahali, kama wengi wa wafuasi wa holiness na Wapentekoste, na Wanazarayo, na Wapilgrim Holiness. Wanaamini kama walipata furaha ya kutosha kucheza, kwamba Hilo ndilo. Na halafu unakata nywele zako, unavaa kaptura? Hivi Roho Mtakatifu angekufanya ufanye hivyo, na huku Yeye analihukumu katika Biblia?

¹⁶³ Vipi ninyi msemao, “Vema, mimi ni mshiriki wa kanisa. Mimi ni Mpentekoste. Mimi ni Mmethodisti, au lo lote nililo. Mimi ni mshiriki! Mama yangu ni mshiriki mwenye cheo kanisani. Mimi nimekuwa mshiriki mwenye cheo”? Na roho yule hasa aliye juu yako anakufanya ufanye mambo ambayo Biblia hii inakukataza wewe kutenda. [Ndugu Branham anagonga mimbara—Mh.] Unaona?

Unasema, “Nimenena kwa lugha, Ndugu Branham. Sasa, usishikilie jambo hilo. Nilinena kwa lugha, na huo ndio uthibitisho wa Roho Mtakatifu.” Kama maisha yako... Iwapo bado unaweza kukata nywele zako, iwapo bado unaweza kufanya mambo haya Biblia inasema usiyafanye; ungeweza kunena kwa lugha mchana kutwa na usiku kuchwa, na bado Mungu hatakujali. Mti hujulikana kwa tunda lake.

¹⁶⁴ Ninazeeka. Ninajua hivyo. Kila siku ninapata maumivu mapya na uchungu. Kila mmoja wetu sisi anazeeka. Afadhali useme kweli. Nilifikiri, “Mungu, usiniache...”

Moja ya mambo ya huzuni sana, ni kumwona mwanamume au mwanamke ambaye hajamkubali Kristo, na aliishi tu kama maskini mshiriki wa kanisa aliyeota kutu, mchoyo

kuliko Shetani mwenyewe, na kumwona nje kule, maskini mtu aliyejaa ukorofi, “Vema, nakuambia, siamini katika...” Mungu kamwe... Hiyo ni—hiyo ni... Hiyo ni taji mbaya sana ambayo Shetani anaweza kuyatia maisha yo yote. Maskini kizee mwanamke aliyejaa manung’uniko, mwenye umri wa kama miaka sitini au sabini, na mikono minene iliyojaa mafuta, na uso uliojaa makunyanzi, na nywele zake zimekatwa, zikiwa na rangi nne au tano mbalimbali, akitembea kwa madaha huku amevaa kaptura ndogo; kama huko si kutiwa taji na Shetani, basi sijawahi kuliona jambo hilo, au mzee mwanamume mwenye hasira kali.

¹⁶⁵ Ee Mungu, najua mimi... Nipe neema nisilalamike kamwe. Nami nataka maisha yangu, Bwana, nataka maisha ya watu wangu... Mungu, jalia kwamba maisha yetu yangeweza kutiwa taji, haidhuru hata tukiteseka, hata iweje, wangapi watanipinga.

Najua jambo hili moja katika maisha yangu, ninapozeeka, rafiki zangu, hao wote walio nyuma yangu, hivi karibuni wataaga dunia, wanazidi kupungua, ninapoendelea njiani. Nami najua jambo moja, hivi karibuni itakuwa kwamba hamna mtu atakayekuja kwangu na kusema... kunitaka shauri. Wale wanijua katika siku za ujana wangu watakuwa wameondoka, kama nitaishi. Rafiki zangu watazidi kupungua, ninapozeeka sasa.

¹⁶⁶ Nami najua siku moja sina budi kufa. Natumaini kwamba Mungu kamwe hatamruhusu Shetani anitie taji kama maskini mzee mwenye kunung’unika, mtu asiyejali, au mke wangu mwanamke mzee mnung’unikaji, au mkeo, ama wewe jinsi hiyo. Ninaomba, ndugu, kwamba maisha yetu yatatiwa taji na matunda ya Roho; upendo, furaha, uvumilivu, upole, subira, Kweli, imani, katika Roho Mtakatifu.

¹⁶⁷ Maisha yangu yanakwisha. Yapata miaka thelathini na mitano iliyopita nilisimama mimbarani hapa, kama mvulana mdogo. Usiku wa leo mimi ni mzee, mvi katika nywele, na kipara, mabega yaliyoinama; nimedhoofika. Maisha yangu yanakwisha, nazo nyuzi ninazotembelea zinakuwa dhaifu. Ninaposomea mbele maishani, rafiki zangu wanazidi kuwa wachache. Na punde si punde itafikia mahali, pengine, kwamba si—sitafurahia nyimbo kama nilivyozea; na labda wajukuu zangu, hao watoto itawalazimu kusema, “Msimsumbue babu.” Inaweza kufikia mahali hapo kama nikiishi.

¹⁶⁸ Kisha nitaendelea kudhoofika hata nisiweze kuinuka kitini mwangu. Halafu asubuhi moja ukungu utaingia chumbani, nitayapungia mkono ng’ambo ya pili, mauti, yaje yanichukue. Yanaweza tu kunishika mkono na kunivusha hadi kwa Bwana wangu. Hayo si msimamizi wa watumwa. Mimi si mtumwa wake. Hayo ni mtumwa wangu. Kristo alishinda mauti kwa ajili yangu.

Na kitu kimoja tu yanachoweza kufanya, ni kunipeleka Uweponi mwa Muumba wangu, “Nyumba ya maskani iliyo ya dunia hii ikiharibiwa.”

¹⁶⁹ Mara mama anapokaribia kuzaa, angalia, mimi sijali yeye amekuwa katili jinsi gani, na jinsi gani alivyo mchoyo. Mnajua, kitambo kidogo kabla huyo mtoto hajazaliwa, huyo mama anakuwa mpole. Ni kwa sababu gani? Wakati hiyo misuli midogo katika hilo tumbo la uzazi inachezacheza na kurukaruka namna hiyo, kuna mwili wa kimbinguni unaomngojea. Na anapotoka kwa mama yake, daktari ama mkunga, ye yote yule yampasa amchukue na kumshtua, anampiga kofi, anamtingisha, au cho chote kile, ndipo anapata pumzi ya uhai. Ndipo roho mdogo wa kimalaika anaingia, pumzi ya uhai, nacho kinakuwa nafsi iliyo hai. Na tunapokuwa na Kristo mioyoni mwetu, na Kristo anakuwa halisi mioyoni mwetu, ni mtoto mchanga. “Nyumba ya maskani iliyo ya dunia hii ikiharibiwa. . .”

¹⁷⁰ Yesu alisema, katika Yohana 14. Katika kufunga, nitasema hivi. Yeye alisema, “Msifadhaike mioyoni mwenu; iwapo manamwamini Mungu, niaminini na mimi. Kwani, katika Ufalme wa Baba Yangu kuna maskani nyingi. Mimi naenda kuwaandalia mahali.” Nyumba ya maskani iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunayo moja. “Mimi nitaenda niwaandalie mahali, ili Mimi nilipo, nanyi muwepo hapo pia.” Tunataka kuwa pamoja Naye.

¹⁷¹ Ndipo najua, wakati mtoto huyu anapolia, kwa kuwa uzao mpya umekwisha umbika, wakati maisha yote mengine yanapoharibika, maisha yote yapatikanayo na mauti na kila kitu kimekwisha, basi itahitajika kitu fulani kunishtua, na inahitaji mauti. Mauti hukupa wewe mshtuko, wakati yanapokupiga, ila tu hukuzaa mara ya pili katika Ufalme mpya, huko ng'ambo ya pili ambako hakuna maradhi, huzuni, hakuna uzee, au cho chote kile. Mungu na atusaidie.

¹⁷² Waweza je, rafiki, waweza je wakati wote ukatae kitu kama hicho, unapoona kwamba hakuna matumaini duniani, nje ya Yesu Kristo? Taa nyekundu zinamemetesha.

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
Ishara ambazo Biblia ilitabiri; (wanawake
wakikata nywele zao, wakivaa kaptura; taa
nyekundu inawaka, unaona)
Siku za mataifa zimehesabiwa, zimekubwa na
huzuni;
“Rudini, enyi mliotawanyika, makwenu.”
Siku ya ukombozi inakaribia,
Mioyo ya wanadamu inazimia kwa hofu;

Jazweni na Roho, mkazitengeneze taa zenu na
zisafishwe,
Inueni macho yenu, ukombozi wenu
umekaribia!

¹⁷³ Nampenda. Nataka nanyi mumpende Yeye. Na wakati tunapoviinamisha vichwa vyetu kwa muda mfupi, katika maombi mafupi, katika kufunga. Taa nyekundu zinamemetesha. Selo inaonyesha. Kuja kwa Bwana kumekaribia. Yeye analizungumzia taifa. Yeye anawazungumzia watu. Anazungumza kwa ishara na maajabu. Nasi tulichukua Sodoma na kuonyesha jinsi yule Malaika alivyomjia Ibrahimu, ishara ambazo Yeye alitenda kabla ya moto kushuka, tunaona hayo.

¹⁷⁴ Yeye alisema, “Katika siku za Lutu, walijenga, waliuza.” Yaangalie mambo hayo siku hizi. “Na kama siku za Nuhu,” wanawake wakiwa warembo, wana wa Mungu wakianguka, miili ya wanadamu ikiabudiwa kwa njia ya wanawake, na mambo haya yote yanayotukia, ambayo tumeyazungumzia usiku wa leo. Taa inamemetesha, Kuja kwa Bwana kunakaribia. Bado wewe ungali mfuasi wa kanisa?

Una hakika, rafiki yangu? Unajuaje utaishi usiku kucha? Mwangelie Ndugu Way amesimama hapa asubuhi hii, mara, akigeuka tu ili apeane mikono na mtu fulani, alianguka akafa papo hapo. Mungu aweza asiwe mwema hivyo kwako hata kukupa nafasi nyingine. Hujui ni dakika ipi ambapo huo moyo utapiga pigo lake la mwisho. Fikiria hilo.

¹⁷⁵ Kuja kwa Kristo kunamemetesha ishara zake. Ziangalie. Angalia kama yale nimewaambieni usiku wa leo... Hayo yawezekana yasipendwe sana na watu, bali ni Ukweli. Ndivyo alivyosema Mungu, na tuko hapa.

¹⁷⁶ Wanawake hawataki kukaa nyumbani. Hawataki kuwatunza jamaa zao. Humwajiri tu yaya kisha wakatoka kwenda kwenye karamu mahali fulani. Hatia za watoto, mambo yote yanatukia; wanakata nywele zao, wanavaa kaptura, kujipodoa. Wanazidi kuwa warembo. Wanaume, wana wa Mungu wanaanguka. Ni mtego wa kutumiwa na Shetani, wana wa Mungu kuanguka katika jambo hilo. Jinsi tu alivyosema Yesu, yabidi litokee. Yeye alisema lingekuwepo, na hili hapa. Yeye alisema, “Mambo haya yatukiapo, kizazi hiki hakitapita,” na hiyo ni miaka arobaini, “hata yote haya yatakapotimizwa.” Waza hilo.

¹⁷⁷ Bado ungali mfuasi wa kanisa? Umetenda kosa? Angalia na ukayachunguze maisha yako, usiku wa leo, enyi wanaume, enyi wanawake. Jichunguzeni, angalieni makosa yenu wenyewe. Vipi, katika hali uliyo nayo hivi sasa, kama Kristo angekuwepo duniani akihubiri haya? Unasema, “Kama—kama Yeye angelikuwepo, kama ningelimsikia Yeye akihubiri hayo, mimi—mimi ningelitubu.” Kama ungelitubu, Hili ni Neno Lake

Mwenyewe usiku wa leo, utafanya hivyo sasa. Kama wewe huna Mungu, na unajua . . .

¹⁷⁸ “Loo,” unasema, “Mimi ni mshiriki wa kanisa. Nimenena kwa lugha. Mimi—mimi si . . .” Sasa tunaweka hilo kando. Jiangalie mwenyewe, yachunguze maisha yako vizuri kwa Neno la Mungu. Je, wewe ni mtu ambaye angeondoka na kusema, “Mimi sijali inachosema Biblia. Ndugu Branham, nadhani umekosea?” Si mimi ambaye nimekosea. Iwapo kuna kosa lo lote kuhusu hilo, Hilo ni Neno.

Nawe haumjui Mungu bado, na huna hakika kwamba kama Yesu angekuja saa hii kwamba ungekuwa tayari kwenda. Kwa nini uchezecheze, na huku unaona mauti yako karibu sana, wakati unapoonza mwisho uko karibu namna hivyo?

¹⁷⁹ Iwapo yupo ye yote hapa, huku vichwa vyenu vimeinamishwa sasa, ungetaka kukumbukwa kwa maombi huku tukimalizia, hebu tafadhali inua mkono wako juu kisha useme, “Ndugu, niombe.” Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki, ndugu, dada. Loo, kila mahali jengoni.

¹⁸⁰ Ndiyo basi, hebu tutoe hesabu kidogo sasa. Ninyi akina dada sasa, kwa uaminifu wote na tumaini, hebu lifikirieni jambo hili. “Hivi kweli nimemtii Mungu? Hasa, shauku yangu iko wapi? Ndugu Branham, ba—ba—ba—bado ningali ninatenda mambo haya. Na—najisikia vizuri. Najisikia mwenye furaha.”

Unajua makafiri hujisikia wenye furaha vivyo hivyo? Je, unajua, mlevi yuna furaha vivyo hivyo, kwa pombe, jinsi ulivyo wewe, kwa ulevi wa pombe? Na iwapo una furaha kwa nguvu ya jambo lo lote ambalo ni kinyume cha Neno la Mungu, ni ibilisi. Kama ukisema, “Nimeridhika kanisani mwangu,” nawe unasikia Neno la Mungu likihubiriwa, nawe hutachukuana na Hilo, umevuviwa na kitu kibaya, haidhuru uvuvio wako ni wa nini. Mimi nimewaona wikipiga makelele, na kurukaruka na kupaza sauti kwa nguvu, na—na kila kitu, na kunywa damu kwa fuvu la kichwa cha binadamu, na kumwita ibilisi, hilo ni kweli, wenye furaha kama vile wewe ungepata kuwa. Ukafiri huonyesha saikolojia kama kitu kingine cho chote, mawazo ya bongoni. Bali ujuzi wa Kristo ni wa moyoni, ambao hubadilisha maumbile yote, humbadilisha mtu akawa kiumbe kipya. Fikiria Jambo hilo, kwa makini sana.

¹⁸¹ Jiangalie mwenyewe. Hebu wazia kioo kikiwa mbele yako, unajiangalia. “Je, mimi ni mwaminifu? Je, mimi ni mnyofu wa moyo? Hivi kweli, moyoni mwangu, ninamtumikia Bwana?”

¹⁸² Sema, “Nalitumikia Hilo.” Angalieni mle ndani, ninyi wanawake mlio na nywele zilizokatwa, mnaovaa kaptura. Jichunguzeni ninyi ambao mnafanya mambo haya. Jichunguzeni enyi wanaume mnaowaruhusu wake zenu wafanye hivyo; mkaseme, “Hivi mimi ni mwana wa Mungu? Hivi mimi ni Msodoma?” Ninyi wanawake semeni, “Hivi kweli mimi ni

mwanamke wa kisasa, au mimi ni baadhi ya kitu kilichotangulia siku za gharika ambacho Yesu alisema kingekuwapo hapa katika siku za mwisho tena?" Lifikirie sana. Jichunguze wewe mwenyewe.

¹⁸³ Unaona, utu wako wewe mwenyewe huonyesha ulivyo. Na iwapo huko sawa, hebu uwe mwaminifu vya kutosha ku... Kuwa mwaminifu sasa, inua mkono wako, useme, "Kristo, simwinulii mkono wangu Ndugu Branham au mtu mwingine isipokuwa Wewe, bali nimekosea. Nisamehe. Ndugu Branham aliahidi kuniombea, sasa nitainua mkono wangu juu, niseme, 'Yesu, nirehemu usiku wa leo. Niokoe kwa ajili ya Kristo. Sitaki kupotea. Uhai huu wote ulionipa Wewe, lingekuwa jambo la kutisha sana iwapo mimi—iwapo nitautupilia mbali tu, ninapokuwa na nafasi hii ya dhamani usiku wa leo kuona kweli kwa macho yangu mwenyewe kwamba taa nyekundu zinamemetesha kila upande; Kuja kwa Bwana, ahadi kwamba Yeye angeonyesha ishara hizi, Naye angewaponya wagonjwa, Yeye angewafufua wafu, angewatoa pepo; kungekuwa na kundi—kundi, watu wachache tu, wachache tu ambao ulimwengu ungewadhihaki, na kuwaita majina mabaya, na kadhalika, namna hiyo."

¹⁸⁴ Basi hawana budi kutuita majina mabaya. Lazima waite Kweli majina mabaya. Yesu alisema, "Ye yote atakayenena neno juu ya Mwana wa Adamu, atasamehewa," wakati Yeye anatenda jambo lile lile unaloliona likitendwa. Akasema, "Bali yeye atakayenena juu ya Roho Mtakatifu, ajapo kufanya jambo lile lile, hasasamehewa katika ulimwengu huu." Unaona, inawabidi wafanye hivyo. Lazima kuwe na Ujumbe kama huo, kuwafanya watu waudhihaki, kuonyesha haki ya Mungu juu ya ulimwengu wote na kuuharibu.

¹⁸⁵ Wakati kuna rehema na mtu fulani akisimama katika pengo, Yesu Kristo, na mlango ulio wazi usiku wa leo, hivi wewe hutampokea Yeye, rafiki yangu?

¹⁸⁶ Sasa, kawaida, ni kuja madhabahuni. Hilo ni sawa. Sina neno dhidi yake. Bali Maandiko, Hayo yalisema, "Wote walioamini walibatizwa." Kwa moyo wako wote, iwapo utasalimisha uhai wako kwa Yesu Kristo papo hapo unapoketi, papo hapo ambapo Yeye alinena nawe ulipoinua mkono wako!

¹⁸⁷ Mungu yeye yule ambaye angeweza kumwita mtu huyu afufuke, akiwa amelala amekufa hapa mbele yangu asubuhi hii, kuwathibitishieni kwamba ninawaambia Kweli. Ni nani anayeweza kufufua wafu ila Mungu? Hiyo ni kweli. Kwa hiyo siye mchungaji wa—wako mdogo aliyechoka hapa, ni Kristo ambaye anakupenda. Naye anakwambia wewe usiku wa leo, "Umesikia Kweli. Umekwisha ona Kweli. Hiyo inatoka katika Neno Langu. Umeliona Neno Langu likifufua wafu. Umeliona Neno Langu likitabiri mambo haya. Umeliona

likitukia sawasawa kabisa katika miaka yote hii, bila kushindwa hata mara moja.”

¹⁸⁸ Sasa utafanya nini na Yesu, wakati kimulimuli chekundu kinamemetesha? Kwa nini usifanye jambo hili, ukitupe chini hicho kipaketi chako cha njugu karanga za kilimwengu! Kwa nini usilitupe chini hilo gazeti la *Hadithi ya Kweli*, na huo u—upuzi wa kale ambamo unabururia nafsi yako kila siku! Kwa nini usiisukumie hiyo televisheni pembeni na kuipindua, iwapo inakuzuia kwenda kanisani! Kwa nini usiweke kando kila mzigo ukuzingao kwa upesi! Kwa nini usimwinulie Kristo moyo wako, ukaseme, “Kristo, usiku wa leo nimeacha yote. Ninajitayarisha. Nakuona Wewe ukija. Ninachukua mzigo wangu, Biblia ya Mungu, ambayo imejaa Uzima wa Milele, na, tangu sasa, nitaishi kwa Hili!” Je, hutafanya hivyo, tunapoomba?

¹⁸⁹ Baba yetu wa Mbinguni, sitaki kuwa mjeuri, kwa hali yo yote, Bwana. Bali Ujumbe huu umeelekezwa kwenye wakati huu, si kwa watu binafsi, si kwa mtu ye yote, bali umeelekezwa kwenye wakati huu. Ndio wakati inaonekana kwamba Roho Mtakatifu ananihimiza kuurekodi huu kwenye ukanda. Kwa maana mara nyingi, mara nyingi humu mimbarani, tumeonyesha siku za Lutu, siku za Sodoma, siku zile ambazo Yesu alinena habari zake, ishara za wakati huu, kuja kwa Bwana, katika njia nyingi. Na halafu baada ya yote yale niliyozungumzia kwa ukali sana dhidi ya wanawake wa siku hizi na nchi nzima, ndipo, Baba, nilifikiri Roho Mtakatifu ndiye aliyenena nami kwamba ningewaelezea watu kwa nini nimetenda jambo hili. Ni kwa sababu Neno Lako lililotiwa pumzi limechungua sana moyo wangu, hata sikuweza kujizuia kamwe.

¹⁹⁰ Yapata karibu mikono hamsini au sabini na mitano humu jengoni iliinuliwa, Baba, kutokana na Neno la Bwana linalokatakata, na ambalo halikunenwa vizuri. Lakini limewafikisha kwenye mshtuko, kuwaacha wajue kwamba filimbi inalia; watakatifu wanakusanyika wote pamoja; mataifa yanavunjika vipande-vipande; ishara za kule Kuja; vimulimuli vyekundu vinamemetesha. Nasi tunaona, kwa kitendo kile, usiku wa leo vimeelekezewa wanawake wetu wa siku hizi, kwamba hivyo ndivyo Biblia ilisema wangekuwa, na hawa hapa basi.

¹⁹¹ Sauti ya Yesu Kristo isiyokosea imetuonya kuangalia siku za Nuhu na kuzilinganisha na siku ambazo tunaishi. Ndipo tukiyaona mambo hayo yakitukia, wanawake wakiwa warembo, na wana wa Mungu wakiwachukua, na jinsi mambo haya yatakavyokuwa, basi tunajua kwamba kizazi kile kitakuona Kuja kwa Bwana. Basi, tunajua kimulimuli kinachomemetesha, kuja Kwake kumekaribia.

¹⁹² Naomba, Baba wa Mbinguni, kwamba Wewe utambariki kila mmoja ambaye ameinua mkono wake. Mimi—mimi ninatoa tu

hii sala nyofu, inayotoka moyoni, na ninajua Wewe utanisikia. Ikiwa Wewe ulikuwa mwema hivyo kwa Ndugu Way asubuhi hii, kuruhusu sala ndogo nyofu kuufanya moyo ule uanze kupiga tena, ya pendo la kweli kwa ndugu ambaye alianguka kwenye paja la mkewe, kiwiliwili baridi ambacho kimekufa. Bwana, jalia watu wajue usiku wa leo kwamba kufa katika dhambi na makosa ni hatari sana kuliko kufa kifo cha mwili; kwani hakuna mtu anayeweza kukuzuia wakati ule, kama ukipita upande wa pili wa pazia, katika dhambi na makosa.

Tujalie usiku wa leo, Bwana, kwamba, kila mtu aliyeinua mkono wake; natoa sala hii katika Jina la Bwana Yesu; kwamba kutakuwa na mabadiliko makubwa maishani mwao, kwamba kutakuwa na kusudi kama hilo mioyoni mwao, kusudi hilo mioyoni mwao kwamba hawatatenda dhambi tena dhidi ya Mungu; kwamba watasimama, tangu hivi sasa, juu ya Neno la Mungu la Milele liliobarikiwa, na walishwe kwa Roho Mtakatifu, awaongoze katika njia za Maisha, siku baada ya siku, wakisafiri kuanzia sasa hivi, na kuendelea.

¹⁹³ Sasa, Baba wa Mbinguni, inawezekana nisiwaone tena, pengine sitaweza kupeana mikono nao kimwili katika dunia hii, ingawa ningelipenda kufanya hivyo. Bali, Bwana Mungu, naomba kwamba sala hii ijibiwe. Nawe ulisema katika Neno Lako, “Yeye ambaye atalisikia Neno Langu, na atamwamini Yeye aliyenipeleka Mimi, yuna Uzima wa Milele; wala hataingia Hukumuni, bali amepita toka mautini kuingia Uzimani.” Katika njia yangu ya unyenyekevu ya kuuleta Ukweli wa Mungu, usiku wa leo, wengi wamelisikia Neno. Sasa, Wewe uliahidi kwamba ungewaokoa, nao “hawatapotea,” kwamba, hakuna mtu angeweza kuwapokonya katika mkono Wako, ya kwamba Wewe ungewafufua siku za mwisho, hakuna hata unywele mmoja wa nywele za vichwa vyao ungepotea. Wewe uliahidi jambo hilo.

¹⁹⁴ Sasa, kama sala, kama mtumishi, Bwana, na kama ndugu kwa—kwao. Na—naomba sala hii na kuwaweka mikononi mwa Mungu, kwamba hawatapatwa na dhara hata moja, na Shetani hatawapokonya katika mkono wa Mungu. Wao ni Wako, ni tunzo. Nami natumaini kwamba Wewe utawapa maisha marefu, na kama ikiwezekana, wape kuona Kuja kwa Bwana Yesu. Na waende toka hapa usiku wa leo, wakafanyike wawaletao watu, kuwaambia wengine, kuwaleta kwenye ujuzi wa wokovu wa Kristo. Tujalie jambo hilo. Yote yamo mikononi Mwako, Baba. Katika Jina la Yesu Kristo.

¹⁹⁵ Na wakati vichwa vyetu vimeinamishwa kidogo. Sijui iwapo mtu kama huyo yupo sasa, ambaye anajisikia kwamba wakati tulipokuwa katika maombi kwamba—kwamba kitu fulani kisicho cha kawaida kimetukia moyoni mwako, na unajisikia kwamba tangu sasa kwamba utaishi maisha ya kujitolea kwa Kristo, na unaona Kuja kwa Bwana kumekaribia, unaamini

yale niliyohubiri ni Kweli, kuhusu hiki kimulimuli chekundu, kuhusu jinsi mambo yalivyo. Na—na unafahamu kwamba ni Neno la Bwana, maana ni Kristo, na unaamini, tangu usiku wa leo utaishi maisha mema na yaliyo karibu na Kristo, kwa sababu ya sala ambayo uliomba usiku wa leo, na ungamo ulilofanya. Na kichwa chako kikiwa kimeinamishwa, hebu inua tu mkono wako, useme, “Ninaamini. Tangu usiku huu, nitaishi maisha tofauti.” Mungu akubariki. Hilo ni nzuri. Hilo kweli ni nzuri sana. Naamini kusema karibu kila mmoja, labda, ambaye aliinua mkono wake muda mfupi uliopita, ameinua mkono wake tena kwamba amelikubali jambo hilo.

¹⁹⁶ Sasa kama hujabatizwa katika Jina la Yesu Kristo upate ondolea la dhambi zako, kumbuka, “Hakuna jina jingine chini ya Mbingu walilopewa wanadamu likupasalo kuokolewa, isipokuwa Jina la Yesu Kristo.” Kumbuka, kuna Bibi-arusi mmoja tu, Bibi-arusi wa Kristo, na huyo amelichukua Jina Lake.

¹⁹⁷ Sasa, na kama hujabatizwa kamwe kwa kuzamishwa majini, katika Jina la Yesu Kristo, hebu mimi kama mtumishi Wake. . . Iwapo Mungu amewathibitishia kwa ishara na maajabu, na kwa Neno Lake, kwamba ninasema Kweli; ninawaamuru kama Mtakatifu Paulo alivyofanya, katika Matendo 19, ambaye alikutana na kundi la Wabatisti. Walikuwa wamebatizwa na Yohana Mbatizaji. Akasema, “Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?”

Wakasema, “Tunajua . . . kama kuna Roho Mtakatifu.”

Akasema, “Basi mlibatizwa kwa ubatizo gani?”

Wakasema, “Tumekwisha kubatizwa tayari, na Yohana Mbatizaji, huko katika Yordani, mtu yule yule aliyembatiza Yesu Kristo.”

¹⁹⁸ Huo ungekuwa ubatizo mzuri sana, lakini Paulo alisema, “Haufai kitu sasa.” Akawaamuru itawapasa kubatizwa tena, katika Jina la Yesu Kristo, Matendo 19:5.

Ndipo Paulo akasema, “Kama Malaika akija kutoka Mbinguni na kuwahubiri injili yo yote isipokuwa Hii ambayo nimewahubiri, na alaaniwe,” Wagalatia 1:8. Kisha akalirudia tena hilo, akasema, “Kama nilivyotangulia kusema, hivyo nasema tena, ‘Ijapokuwa Malaika,’ sembuse mhudumu, askofu, papa, au cho chote kile, “Kama Malaika akishuka toka Mbinguni, Ke—Kerubi kutoka Mbinguni, na kuwahubiri injili nyingine isipokuwa Hiyo, na alaaniwe.”

Basi, nawaamuru, iwapo hamjabatizwa katika Jina la Yesu Kristo, wakati maji yako kwenye kidimbwi, na mavazi yanangojea, njoni mkabatizwe, “Mkiliita Jina la Bwana, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu; kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa watu wote

walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

¹⁹⁹ Baba yetu wa Mbinguni, sasa jambo hili liko mikononi Mwako. Kumshawishi mtu, ninajaribu; bali kumfanya mtu, siwezi. Na Wewe hutendi dhidi ya mapenzi ya mwanadamu; kwa sababu, kama mwanamume au mwanamke amechaguliwa tangu asili kwa ajili ya Uzima wa Milele, wakati Nuru ya Mungu inapomemetesha juu ya mbegu ile, itapata Uzima. Na kama kuna Uzima miongoni mwetu usiku wa leo, Baba, ambao Wewe uliumemeteshea Nuru Yako, nao wameona Kweli, hebu na waende kwa unyenyekevu na kwa furaha kwenye kidimbwi, wakabatizwe katika Jina la Mwanao mpendwa, Yesu Kristo.

²⁰⁰ Ambapo, tunajua kwamba kila mtu katika Maandiko ilimbidi kubatizwa, na kubatizwa tena. Wale ambao hawakubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, iliwabidi wabatizwe tena. Na yule mtume maarufu, ambaye alikuwa na funguo za Ufalme, alisema kwenye Siku ya Pentekoste, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, ili dhambi zenu zipate kuondolewa, ndipo ahadi ya Roho Mtakatifu ni kwa ajili yenu.” Tujalie kwamba itatimizwa usiku wa leo, kwa utimilifu wote, Baba.

²⁰¹ Ninawatoa Kwako sasa. “Chukua maneno haya machache na mawazo ya moyo wangu, na yapate kibali machoni Pako, Ewe Bwana.” Na yatie nanga kwa watoto Wako, yawape Uzima wa Milele. Waokoe wote wale ambao ni wa kuokolewa, na uwaponye walio wagonjwa. Hebu neema ya Mungu ikae juu ya kila mmoja wao, wakati tunapowatoa Kwako sasa, katika Jina la Yesu.

²⁰² Sasa huku vichwa vyetu vikiwa vimeinamishwa, nitamwomba dada yetu ambaye anacheza piano aje hapa. Kwa dakika moja, kama dakika tano zaidi. Na kama yupo ye yote ambaye anatamani kubatizwa sasa, ambaye ametubu na kuamini. Kama unaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, na unaamini jambo lilo hilo kwa moyo wako wote, sio tu—msisimko tu, bali unaliadini, na uko tayari kuungama kwamba umekosea; na haategemei ustahifu wako mwenyewe, kichu juu ya yale Yeye ametenda; na uko tayari kuja huku mwenye, kuchukua Jina Lake katika ubatizo wa maji, upate kuwa kiungo cha ule Mwili kwa Roho Mtakatifu; basi, chumba cha wanawake kiko kwenye mkono wangu wa kuume, na chumba cha wanaume kiko katika mkono wangu wa kushoto, na majoho na kadhalika tayari.

²⁰³ Huku tumeinamisha vichwa vyetu, wakati dada yetu anacheza piano, “Nasikia Mwokozi akiita,” iwapo kiongozi wa nyimbo atatupa neno dogo la huo. Vichwa vyetu vikiwa vimeinamishwa sasa, ibada iko mikononi mwa Mungu Mwenyezi sasa; kwa ye yote anayetaka kubatizwa; anayetaka kwenda kwenye vyumba vya maombi kuomba dua kwa ajili ya ubatizo

wa Roho Mtakatifu, kuna wakufunzi hapa watakuwa tayari kuwafunza au kufanya kitu cho chote. Na Maneno hayo yasianguke bure, bali na yatimize yale ambayo yalikusudiwa. Vichwa vyetu vikiwa vimeinamishwa, hebu na tuombe sasa. Na, na akuongozako Yeye, mfuata.

Nasikia Mwo...(Sasa omba, kila mwenye dhambi.)

Nasiki Mwokozi...(Je, ungeweza kumsikia Yeye akiita, alipomfufua mtu aliyekuwa amekufa asubuhi hii?)

Nasikia...(Je, ungeweza kumsikia Yeye akiita, anaposikia Neno Lake likimemetesha Nuru Yake wakati wa mwisho?)

Nitamfuata, mfuata...(Unakubali kumfuata kote?)

Aniongozako...(Mungu akubariki, ndugu yangu. Wanaume upande wa kushoto. Wanawake wa kulia.) Na...

Aniongozako nitamfuata,

Aniongozako...(Biblia ilisema, "Wote walioamini walibatizwa.")...mfuata,

Nitamfuata, mfuata kote.

Nitamfuata bustanini,

Nitamfuata bustanini,

(Roho Mtakatifu...?...))

Nitamfuata busta...

Ikiwa mtu fulani atafuatana na wanawake upande huu, kwa ajili ya kumtafuta Roho Mtakatifu, ingieni katika chumba cha mkono wa kulia, baadhi ya ninyi dada mliofunzwa na Bwana.

...kote.

Aniongozako...

Je unaweza kwa uaminifu kusema kwamba, "Aniongozako nitamfuata"? Je, utatenda jambo hilo? Vipi kuhusu Sauti ile ndogo inayozungumza nawe, utaenda—utaenda ambako Yeye anakuongoza? Angalia ile taa nyekundu. Unaona ile taa ikimemetesha? Tuko kwenye wakati wa mwisho.

Aniongozako nitamfuata,

Nitamfuata, mfuata kote.

Nasikia Mwokozi akiita...

Yeye huzungumzaje? Kupitia kwa Neno Lake, moyoni mwako. Je, utakuja sasa? Huu ni mwaliko wako. Kumbuka, kama likitukia kabla hatujakusanyika pamoja tena, umekwishaonywa.

...sikia Mwokozi akiita,

"Twa msalaba wako unifuata."

Aniongozako...

Sasa tafadhali baadhi ya ndugu, kwa ajili ya mafundisho, waingie kwenye chumba hiki hapa kwenye mkono wangu wa kushoto, ndugu wakijitayarisha kwa ajili ya ubatizo. “Aniongozako...” Baadhi ya ndugu wahudumu hapa, njoni mtusaidie, ingieni chumbani pamoja nao.

...mfuata,
Aniongozako...(Kweli unamaanisha jambo hilo?) mfuata,
Nitatamfuata, mfuata kote.

²⁰⁴ Sasa, ngojeni kidogo. Sasa, kama hujabatizwa majini, kwa kuzamishwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Kwa vyeo tu, “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” hapajawahi kuwa na mtu kamwe katika Biblia nzima, hata mtu mmoja, aliyewahi kubatizwa katika Biblia, katika Jina la “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” katika cheo hicho. Hakuna mtu aliyewahi kubatizwa kanisani, katika historia, kwa miaka ya kwanza mia tatu upande huu, kila mmoja alibatizwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo, mpaka kwenye Baraza la Nikea huko Nikea, Rumi, ambako kanisa la Kikatoliki la Kirumi lilipounda madhehebu, ndipo wakaweka badala yake vyeo vya “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.”

²⁰⁵ Kama kuna mwanahistoria, mhudumu, mtu ye yote, hewani, kwenye kanda, ambaye anaweza kutoa Andiko moja au chembe moja ya historia, ambapo mtu ye yote amewahi kubatizwa kwa njia yo yote isipokuwa katika Jina la Yesu Kristo, hadi kanisa Katoliki la Kirumi hapo Nikea, Rumi, unawajibika kuniletea kisa hicho, nami nitaomba radhi. Hakuna kitu kama hicho. La. Na kila mtu aliyebatizwa kwa kuzamishwa majini, ambaye hakubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, aliamriwa, kabla ya kuweza kuingia Utukufuni, kurudi akabatizwe tena. Sasa ni juu yako.

²⁰⁶ Hakuna Andiko katika Biblia, ambapo mtu ye yote aliwahi kubatizwa, akitumia jina la “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” kama watu wanavyobatiza leo. Ni Kikatoliki, kanuni ya imani ya Katoliki ya Kirumi ambayo ilipokezanwa kupitia Martin Luther, na John Wesley, ikaendelezwa mbele. Na Biblia inabashiri ingekuwa namna hiyo, na itaishia katika siku za mwisho, na mlango ungefunguliwa, kama tulivyopitia hivi majuzi katika nyakati za kanisa kuliona jambo hilo.

²⁰⁷ Ni juu yako. Mimi ni mjumbe tu wa Ujumbe huu. Mara nyingine tena, hebu na tuuamini. Milango iko wazi. Sehemu ya kubatizwa imejaa, na hakuna sababu... Kuna mavazi tayari, na tutakuwa tayari kubatiza mnamo dakika chache zijazo.

²⁰⁸ Iwapo upo hapa na hujabatizwa, mara nyingine tena hebu na tuimbe, nawe njoo, je, utakuja? Timiliza...

²⁰⁹ Unasema, “Ninakusudia kufanya jambo hilo siku moja, Ndugu Branham.” Hiyo siku moja huenda ikakufikia kama

ilivyofanya kwa Ndugu Way asubuhi ya leo, lakini labda pasipo kufuatiwa na neema, kama ilivyotendeka. Unaweza kuondoka dakika yo yote. Aidha wewe ni kijana, kama utamaliza usiku huu ukali hai, uta... Na iwapo una umri wa miaka sabini, utaishi kuliko wengi wenye umri wa miaka thelathini. Maelfu yao watakufa usiku huu. Hiyo ni kweli. Wewe hujui utaondoka lini.

²¹⁰ Uwe na hakika. Usibahatishe jambo hilo. Hebu kumbuka, unaweza kubahatisha kazi yako, au kubahatisha jambo *hili*. Bali usibahatishe juu ya jambo Hilo. Kumbuka, sauti yangu itakuwa shahidi kwenye kanda ya sumaku ya Mungu katika Siku ya Hukumu, dhidi yake.

²¹¹ Bali sasa fikiria jambo hilo, tunapoimba tena huku vichwa vyetu vimeinamishwa. “Aniongozako...” Ndugu Neville. “...Nitamfuata.”



KIMULIMULI CHEKUNDU CHA DALILI YA KUJA KWAKE SWA63-0623E

(The Flashing Red Light Of The Sign Of His Coming)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni Juni 23, 1963, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2011.

SWAHILI

©1991 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org